# Kwa Kupigwa Kwake

## Je, kusulubiwa pamoja na Kristo kunamaanisha nini?



Bill Pinto

## SURA YA 1

Kwenye kitabu cha Waebrania kuna mstari ambao hauwezi kueleweka kirahisi sana pale Mkristo yeyote wa uinjilisti anapousoma. Badala yake, unaweza tu kueleweka kupitia mtazamo wa mahali patakatifu pa mbinguni, huduma ya ukuhani mkuu wa Kristo, na upatanisho. Kwa hiyo, aya hii inawavutia sana Waadventista Wasabato.

> "Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu." Waebrania 9:28

Ni ukweli kuwa mwenye dhambi anapata msamaha na kuhurumiwa kupitia msalaba. Isipokuwa ni kwamba, dhambi zetu zinabakia kwenye kumbukumbu mpaka wakati wa kutakaswa kwa mahali patakatifu pa mbinguni, ambapo kunaashiria mwisho wa hukumu na ujio wa Yesu Kristo atakayekuja muda si mrefu. Hivi ndivyo Paulo anavyomaanisha anapoelezea kuja kwa Kristo mara ya pili kuwa ni kuja "pasipo dhambi". Kristo hawezi kurudi mpaka kumbukumbu la dhambi isafishwe kutoka mahali patakatifu pa mbinguni. Hapo ndipo Kristo "atakapotokea mara ya pili pasipo dhambi" na kuleta wokovu kwa wale ambao wamekuwa wakimtafuta Yeye.

Je, ni nini kinachopaswa kufanyika ili mahali patakatifu pa mbinguni patakaswe?

Ni lazima dhambi zote zisafishwe kutoka kwenye mioyo ya wale wanaoishi kwenye siku za mwisho. Kwa hiyo, Kristo anapofanya kazi ya kuwasafisha watu wake kutoka kwenye dhambi, mtu aliye duniani ambaye anaamini anapaswa kutoa ushirikiano kwenye hii kazi.

Sio kwa bahati, kutakaswa kwa kumbukumbu ya dhambi kutoka mahali patakatifu pa mbinguni kunahusiana kwa ukaribu na siku ya upatanisho katika Agano la Kale. Hebu fikiria maagizo ya Mungu kwa makuhani kuhusu tukio hili.

> "Kwa maana siku hiyo upatanisho utafanywa kwa ajili yenu, ili kuwa-

> takasa; nanyi mtatakaswa na dhambi zenu zote mbele za BWANA.
>
> Ni Sabato ya raha ya makini kwenu nanyi mtajitaabisha roho zenu; ni amri ya milele." Mambo ya Walawi 16:30-31

Siku ya kawaida ya upatanisho ilikuwa ni siku ambayo kumbukumbu ya dhambi ilisafishwa kutoka mahali patakatifu pa duniani, "ili [mtu] apate kutakaswa na dhambi [zao] zote mbele za BWANA." Kwa hiyo walipaswa kuzitesa nafsi zao milele kwa kuzifuata amri. Watu waliamriwa hivi:

> "Nanyi msifanye kazi yoyote siku hiyo; kwa kuwa ni siku ya upatanisho, ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu mbele za BWANA, Mungu wenu. Mambo ya Walawi 23:28
>
> "Itakuwa kwenu Sabato ya kustarehe kabisa, nanyi mtazitesa nafsi zenu; siku ya kenda ya mwezi wakati wa jioni, tangu jioni hata jioni, mtaishika hiyo Sabato yenu." Mambo ya Walawi 23:32

Wakati kuhani alipokuwa akikamilisha kazi hii ya utakaso, mtu anayeamini—kupitia imani kwa kuhani mkuu—alipaswa kutesa nafsi yake.

Inamaanisha nini mtu kutesa nafsi yake? Sehemu hii inaelezea neno hilo kama kujishusha wewe mwenyewe. Ni kunyenyekea, kujishusha zaidi na kujirudia wewe mwenyewe. Wakijua kwamba asili yao ya ubinafsi ilikuwa inawaongoza kuelekea kwenye dhambi, watu wa Mungu walipaswa kusalimisha nafsi zao, kujinyenyekeza na kujishusha sana wakionyesha huzuni kwa ajili ya dhambi zao, na hivyo, kushiriki kwenye kazi ambayo kuhani mkuu alikuwa akikamilisha. Na kwa wale ambao hawakususha nafsi zao, sheria ilisema hivi:

> "Kwa kuwa mtu awaye yote asiyejitesa mwenyewe siku hiyo hiyo, atakataliwa mbali na watu wake." Mambo ya Walawi 23:29

Vivyo hivyo, kwenye muktadha wa siku isiyo ya kawaida ya upatanisho, kitabu cha Waebrania 9:28 kinawaelezea watu "wanaomtafuta";

Kuhani wao Mkuu na Mwokozi wao. Kundi hili pia lipo nje ya mahali patakatifu wakitesa nafsi zao. Yesu (Kuhani wao Mkuu) anapofanya upatanisho kwa ajili yao na kuwatakasa kutoka kwenye dhambi, hawa wachache wanaomcha Mungu wanajinyenyekeza na kujishusha sana; wakishirikiana na kazi ambayo Kristo anaikamilisha kule mbinguni.

Kwa nini jambo hii ni la muhimu?

Kwa sasa, Kristo ako mahali patakatifu pa mbinguni, akifanya huduma kama Kuhani wetu Mkuu na kufanya upatanisho kwa ajili yetu. Lakini, kama Paulo alivyosema; Kristo atarudi bila dhambi kwa ajili ya wokovu. Rekodi ya dhambi itasafishwa. Na kisha, wale ambao hawashirikiani na kazi ya Kristo kwa kutozitesa nafsi zao na kujinyenyekeza watakataliwa kwenye kutaniko. Ndiyo maana kwenye kitabu cha Waebrania 9:28, Paulo anatuelekeza kwa watu "wanaomtafuta". Nafsi hizi zinazomtazama Kristo zinajitesa zenyewe, na hao ndio ambao Kristo atawatokea mara ya pili. Bila shaka, wanafuata mapenzi ya Mungu kila sehemu ya maisha yao. Wanasalimisha nafsi zao na kudhihirisha imani katika Kristo.

> SWALI: Je, kumbukumbu ya dhambi inafikaje mahali patakatifu pa mbinguni?

Kwanza kabisa, tuchunguze mahali patakatifu pa duniani, ambapo Mungu alipatoa kama mfano (au uwakilishi) wa mahali patakatifu pa mbinguni.

Kulikuwa na njia mbalimbali ambazo rekodi ya dhambi ingeweza kuhamishwa mpaka mahali patakatifu pa duniani, ikitegemea mtu na aina yake ya dhambi. Kwa mfano, kwenye kisa cha kuhani ("kutaniko la mahali patakatifu"), makuhani au wazee wa kutaniko waliagizwa kuchukua ng'ombe dume kwa ajili ya toleo la dhambi. Kitabu cha Mambo ya Walawi 4:6 kinaeleza kile ambacho kuhani alipaswa kukifanya na dhabihu hiyo ya mnyama.

> "kisha kuhani atatia kidole chake katika hiyo damu na kuinyunyiza damu mbele ya BWANA mara saba, mbele ya pazia la mahali pa-

takatifu." Mambo ya Walawi 4:6

Mara tu dhambi ilipoungamwa juu ya dhabihu tajwa, mnyama aliuawa (aliyebeba dhambi hiyo), na damu ilinyunyiziwa mbele ya pazia la mahali patakatifu. Kwa hiyo rekodi ya dhambi ilihamishwa kutoka kwa kuhani hadi kwenye dhabihu na hatimaye hadi mahali patakatifu.

Maagizo zaidi yanatolewa kwenye mistari ya 14-17, ambapo hali iliyopo ilihitaji kutaniko itoe fahali kwa ajili ya dhambi zao.

> "hapo Itakapojulikana hiyo dhambi waliyoifanya, ndipo mkutano utatoa ng'ombe mume mchanga awe sadaka ya dhambi, na kumleta mbele ya hema ya kukutania.
>
> Kisha wazee wa mkutano wataweka mikono yao kichwani mwake huyo ng'ombe mbele za BWANA;
>
> kisha ng'ombe atachinjwa mbele za BWANA. Kisha kuhani aliyetiwa mafuta atatwaa katika damu ya huyo ng'ombe na kuileta ndani ya hema ya kukutania;
>
> kisha kuhani atatia kidole chake katika hiyo damu, na kuinyunyiza mbele za BWANA, mbele ya pazia mara saba."
> Mambo ya Walawi 4:14-17

Kwa mara nyingine tunaona jinsi rekodi ya dhambi inavyoweza kuhamishiwa kwenye mahali patakatifu pa dunia. Mistari ifuatayo inatuonyesha njia nyingine ambayo rekodi ya dhambi inaweza kuhamishwa; kwa kula sadaka ukiwa pale mahali patakatifu.

> "Nena na Haruni na wanawe, uwaambie, Amri ya hiyo sadaka ya dhambi ni hii; mahali hapo pachinjwapo sadaka ya kuteketezwa ndipo itakapochinjwa sadaka ya dhambi, mbele za BWANA; ni takatifu sana.
>
> Huyo kuhani atakayeisongeza kwa ajili ya dhambi ndiye atakayeila; italiwa katika mahali patakatifu, katika ua wa hema ya kukuta-

> nia." Mambo ya Walawi 6:25-26

Iwe ni kwa kunyunyiza damu mbele ya pazia, au kwa kula sadaka ya dhambi ukiwa mahali patakatifu, kumbukumbu ya dhambi inahamishiwa mahali patakatifu. Kisha, kwenye siku ya upatanisho, kuhani angesafisha patakatifu pa kidunia kutoka kwenye kumbukumbu ya dhambi ambayo ilikuwa imekusanywa mwaka uliopita.

Ni muhimu kutambua kuwa nadharia mbalimbali ambazo Mungu alimpatia Musa zilipaswa kufuatwa kwa umakini na kwa uwangalifu. Kama ambavyo kitabu cha Mambo ya Walawi 10 kinaweka bayana, kuhani asipozitii amri hizi, alikuwa anajiletea adhabu ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Fikiria wana wa Haruni, Nadabu na Abihu, ambao waliangamizwa mara moja kwa kumtolea Bwana moto haramu ambayo Mungu hakuwa ameamuru. Hadithi hiyo inapoendelea, tunaona kuwa Haruni na wanawe wengine wawili, Eleazari, na Ithamari, walipaswa kuendelea kufanya kazi kwenye mahali patakatifu siku hiyo kulingana na maagizo ya Mungu yaliyo wazi.

> "Kisha Musa akanena na Haruni, na Eleazari na Ithamari, hao wanawe waliobaki, Twaeni hiyo sadaka ya unga iliyosalia katika kafara za BWANA zilizotolewa kwa moto, mkaile pasipo kutiwa chachu, pale karibu na madhabahu; kwa kuwa ni takatifu sana;
>
> nanyi mtaila katika mahali patakatifu, kwa sababu ni haki yako, na haki ya wanao, katika hizo kafara zisongezwazo kwa BWANA kwa moto; kwanini hivyo nilivyoagizwa." Mambo ya Walawi 10:12-13

Kupitia Musa, Mungu aliwaagiza makuhani waendelee na kazi yao. Kwa hakika, mistari ya awali inafichua kuwa hawakuruhusiwa hata kuomboleza kifo cha Nadabu na Abihu ama sivyo nao wangekufa. Badala yake, kwa heshima ya utakatifu wa kazi ya upatanisho, waliamriwa kula sadaka ya dhambi wakiwa mahali patakatifu. Baada ya kutoa maagizo haya, Musa akarejea kutazama endapo Haruni na wanawe walikuwa wamezitii amri za BWANA.

> "Kisha Musa akamtafuta sana huyo mbuzi wa sadaka ya dham-

bi, naye, tazama, alikuwa amekwisha kuchomwa moto; naye akawakasirikia hao Eleazari na Ithamari, wana wa Haruni, hao waliobaki, akawaambia

Kwa nini hamkula hiyo sadaka ya dhambi katika mahali patakatifu, kwa kuwa ni takatifu sana, naye amewapa ninyi ili kuuchukua uovu wa mkutano, na kuwafanyia upatanisho mbele za BWANA?

Angalieni, hiyo damu yake haikuletwa ndani ya mahali patakatifu; iliwapasa kuila ndani ya mahali patakatifu, kama nilivyowaagiza." Mambo ya Walawi 10:16-18

Jukumu la makuhani—kufananisha kazi ya Kristo—lilikuwa ni kula dhabihu ya dhambi ukiwa mahali patakatifu kwa sababu hivyo ndivyo wangebeba uovu wa kutaniko, na hivyo kufanya upatanisho kwa ajili yao mbele za Bwana. Ingawa sababu ya Haruni kutofanya hivyo ilikubaliwa wakati huu (kama mistari ya 19-20 inavyoonesha) hadithi hii inadhihirisha uhakiki uliohudhuria kazi ya upatanisho kwenye Agano la Kale.

Kwa kuuchukua uovu wa kutaniko, kuhani alikuwa akifanya upatanisho kwa ajili ya watu. Hii ndiyo kazi ambayo Kristo anaikamilisha kule mbinguni. Hata sasa, anabeba dhambi zetu mbele za Baba na kufanya upatanisho kwa ajili ya watu wake. Kazi hiyo itakapokamilika, Kristo atarudi "pasipo dhambi" kwa ajili ya wokovu; asichukue tena uovu wa kutaniko. Zaidi ya hayo, kwa kuwa makuhani walipaswa kubeba dhambi za watu, tazama namna ambavyo kuhani alipaswa kuwa.

"Wala hamtatoka nje mlangoni mwa hema ya kukutania, msije mkafa; kwasababu mafuta ya kutiwa ya BWANA ya juu yenu. Nao wakafanya kama hilo neno la Musa." Mambo ya Walawi 10:7

Kupakwa mafuta kwa makuhani lilikuwa ni jambo nzito sana. Kwa kuwa kuhani alikuwa ni mfano wa Kristo, ilimbidi naye awe ni mtakatifu.

"kisha, mpate kupambanua kati ya yaliyo matakatifu na hayo

> yaliyo ya siku zote, na kati ya yaliyo najisi na hayo yaliyo safi;" Mambo ya Walawi 10:10

Hiyo ndiyo sababu hasa ya kusababisha Nadabu na Abihu kupigwa. Walikichukulia kitu ambacho kilikuwa ni kitakatifu kana kwamba ni kitu tu cha kawaida. Mungu asingeweza kukubali huduma ya aina hiyo. Ingawa makuhani walikuwa wanadamu wanaoweza kufa, walikuwa wakimwakilisha Kristo; Kuhani Mkuu wa kweli ambaye ni mtakatifu na asiye na dhambi.

Katika kitabu cha Mambo ya Walawi 21, kuna sifa ambazo zimetolewa kwa washiriki wa ukuhani. Kuhusu kuhani mkuu imesemwa hivi:

> "Na yeye aliye kuhani mkuu katika nduguze, ambaye mafuta ya kutiwa yamemiminwa kichwani mwake, naye akawekwa wakfu ili ayavae hayo mavazi, yeye hataziacha wazi nywele za kichwa chake, wala hatazirarua nguo zake;
>
> wala asitokee katika mahali patakatifu, wala asipatie unajisi mahali patakatifu pa Mungu wake; kwa kuwa utakaso wa hayo mafuta ya kutiwa ya Mungu wake yu juu yake; mimi ndimi BWANA."
> Mambo ya Walawi 21:10,12

Ni muhimu kuzingatia kwamba sio Walawi wote wangeweza kuhudumu mahali patakatifu. Vigezo fulani vya kimwili, kiakili na kiroho vilipaswa kutimizwa kwanza. Kutiwa mafuta kama kuhani ilikuwa ni jambo nzito sana kwa sababu kuhani alikuwa akimuwakilisha Kristo. Hawakupaswa kuishi kwa njia ya kawaida kama watu wengine walivyokuwa wanaishi, bali waliwekwa kando kwa kusudi fulani. Kifungu kifuatacho kinaeleza mojawapo ya sifa za kimwili ambazo kuhani alipaswa kuwa nazo.

> "Mtu awaye yote kwa kizazi cha Haruni kuhani aliye na kilema asikaribie kuzisongeza sadaka za BWANA kwa njia ya moto; ana kilema huyo asikaribie kusongeza chakula cha Mungu wake.
>
> Lakini hataingia ndani ya pazia, wala asikaribie madhabahu, kwa

> sababu ana kilema; ili kwamba asipanajisi patakatifu pangu; kwa kuwa mimi ndimi BWANA niwatakasaye."
> Mambo ya Walawi 21:21,23

Mungu hakuwa akibagua muonekano wa mtu kwa kusudi la ubatili. Badala yake, vigezo hivi vilitolewa ili kufichua utakatifu wa kazi ya ukuhani kwenye kila jambo.

Kwenye kitabu cha Waebrania 7:26, Paulo anamfafanua Yesu na kusema hivi: "Maana ilitupasa sisi tuwe na kuhani mkuu wa namna hii aliye mtakatifu, asiyekuwa na uovu, asiyekuwa na waa lolote, aliyetengwa na wakosaji, aliyekuwa juu kuliko mbingu;" Hivyo ndivyo namna ambavyo vigezo kwenye kitabu cha Mambo ya Walawi vilikuwa vinaelekeza. Makuhani walipoyapokea mafuta ya upako, walikuwa wakimuwakilisha Yeye; mtakatifu, asiye na madhara, asiye na uchafu na aliyejitenga na wakosefu. Na hapo ndipo makuhani wangeweza kushiriki kwenye dhabihu na kufanya upatanisho kwa ajili ya watu. Unaona, hii njia ya mifano inaonesha kwamba kuhani alikuwa amebeba dhambi za watu. Na kwa hivyo Mungu aliwapa maagizo maalum ya kurekebisha kila sehemu ya maisha yao.

## SURA YA 2

Wakati mtu alipotenda dhambi, alipaswa kuweka mkono wake juu ya dhabihu ya mnyama ili kuhamishia dhambi yake kwa huyo mnyama. Baada ya mnyama kuuawa, damu yake ilinyunyizwa juu ya pazia na madhabahu kwenye mahali patakatifu. Katika nyakati fulani, kuhani angekula dhabihu hiyo, akibeba dhambi kwenye mahali patakatifu.

Sasa kuna maswali mawili ya muhimu. Sadaka inamuwakilisha nani? Na kuhani mkuu anamuwakilisha nani?

Wote wawili wanamuwakilisha Yesu. Dhabihu na kuhani mkuu ni mifano ya Kristo. Fikiria sadaka ya kuteketezwa kama mfano.

> “Kisha ataweka mkono wake juu ya kichwa cha hiyo sadaka ya kuteketezwa; nayo itakubaliwa kwa ajili yake ili kufanya upatanisho kwa ajili yake.” Mambo ya Walawi 1:4

Mungu anaikubali sadaka ya kuteketezwa kwa niaba ya mwenye dhambi aliyetubu. Kama Musa anavyoandika kuwa, "imekubaliwa kwa ajili yake ili kuleta upatanisho kwa ajili yake". Ni dhabihu ya Kristo ambayo inafanya upatanisho kwa ajili yetu. Lakini daima hiyo sadaka ya kuteketezwa ilikuwa inatakiwa kuteketezwa wakati wa mchana na usiku; ikiwakilisha maombezi yasiyokoma ya Kristo kwa ajili ya mwanadamu. Angalia ni nini kingine kinachooneshwa na kuhani mkuu kwenye mahali patakatifu pa duniani.

> “Nawe utie hizo Urimu na Thumimu katika kile kifuko cha kifuani cha hukumu; nazo zitakuwa juu ya moyo wa Haruni, aingiapo mbele za BWANA; na Haruni atachukua hukumu ya hao wana wa Israeli juu ya moyo wake mbele za BWANA daima.” Kutoka 28:30

Siku zote majina ya wana wa Israeli yalikuwa moyoni mwa kuhani mkuu. Pia, huyu ni muwakilishi wa Kristo anayebeba majina yetu kwenda mbele za Baba wa Mbinguni. Kristo anawawakilisha wale wanaomtazama na kumfuata kwa imani. Na hili si jambo ambalo Mwana wa Mungu anahisi kutokuwa na hisia nalo. Jina lako imo moyoni

mwake. Hivyo ndivyo Kristo anavyotaka kukuokoa. Fikiria huu mfano Anaoutoa kupitia nabii Isaya:

> "Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe." Isaya 49:15

Ili kuonyesha vizuri zaidi upendo Wake kwa wanadamu, Mungu anajipambanua kutoka kwenye kielelezo kikuu cha upendo kwenye ulimwengu huu: mama mlezi. Kisha anauliza swali ambalo mtu hatafikiria kuliuliza. Mama mwenye upendo angefanya lolote kwa ajili ya mtoto wake; angetoa uhai wake kwa ajili ya mtoto wake. Lakini Bwana anasema kwamba upendo Wake kwako ni mkuu zaidi ya huu. Anasema kuwa mama anayenyonyesha "aweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe". Hiyo ndiyo maana ya kuhani mkuu kuyabeba majina ya Israeli kwenye moyo wake.

Kwenye mstari unaofuatia, Mungu anasema: "Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu; kuta zako ziko mbele zangu daima." Isaya 49:16. Kristo anajiunganisha nasi kwa ukaribu sana ingawa kimwili Yupo mbinguni, tunaambiwa kuwa Yupo nasi kama vile Alipokuwa akitembea duniani. Anajidhihirisha kwenye mateso yetu, huzuni zetu, na majaribu yetu. Na ndani ya moyo wake kuna majina ya wana wa Israeli wa kiroho ambayo Kristo amebeba kabla ya hukumu. Kisha, wakikubaliwa mbele za Baba, watu waliomo moyoni mwake wanakubaliwa ndani Yake.

> "Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa." Waefeso 1:6

Wakati Paulo alitoa kauli hii kwenye Agano Jipya, ingewahusu hasa Wayahudi waliopotea. Wayahudi walielewa maana ya huduma ya mahali patakatifu na siku ya upatanisho. Walielewa kuwa kuhani mkuu alipotoka patakatifu pa patakatifu walikubaliwa ndani yake, kwa maana kuhani alikuwa ameyataja majina yao mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu.

Kukubalika kwa mpendwa kunamaanisha nini?

> "Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake." Waefeso 1:7

Kukubalika kwa mpendwa ni mtu kusamehewa dhambi. Hii ndiyo kazi ambayo kuhani mkuu anajishughulisha nayo anapoyabeba majina ya Israeli moyoni mwake. Anatafuta upatanisho kwa ajili ya dhambi zao. Vivyo hivyo, Baba anapomtazama Mwanawe (akiwa amebeba jina lako moyoni mwake), unakubaliwa ndani ya Yesu na unapokea msamaha kupitia damu yake. Dhabihu ya Kristo inatolewa kwa niaba yako. Ndio maana tukaona kuwa siku ya upatanisho watu wazitese nafsi zao; kujidhili, kujikana na kunyenyekea. Iliwabidi kukiri imani yao katika Kristo ili wakubalike katika Kristo. Na kwa damu yake wangepokea msamaha wa dhambi.

Kristo ndiye mwakilishi wetu mbele za Baba patakatifu pa mbinguni. Hata hivyo amekuwa akituwakilisha maisha Yake yote. Hii inatumika si tu kwa Wakristo, bali kwa watu wote. Kwenye maisha Yake yote—mateso, kifo, kuzikwa na kufufuka kwake—Yesu alikuwa akiwawakilisha wanadamu wote. Kwa hiyo, unapokaa maisha yaliyo kamili ya Kristo, mfikirie akiishi maisha hayo kwa niaba yako. Iwe ni kama alikuwa akiteseka chini ya majaribu au mateso, au hata kusulubiwa, yote yalikuwa yakiendelea kwa niaba yako. Utii wa Kristo ulikuwa ni kwa ajili yako. Mateso yake, kifo, ufufuo, utukufu na maombezi yake yote yalikuwa ni kwa ajili yako. Hilo ndilo jukumu ambayo kuhani mkuu wa duniani alitakiwa kuhusika nalo.

Ni lazima mtu azingatie sana aina ya lugha mitume hutumia wanapozungumza juu ya Kristo. Zingatia kwamba hawazingatii mateso Yake kuwa ni tofauti na yetu.

> "Na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; maana, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye." Warumi 8:17

Paulo anasema hivi: “tukiteswa pamoja naye”. Yesu hateseki tena kama ilivyokuwa wakati Alipokuwa duniani. Paulo anazungumzia wakati uliopo. Anafanya hivyo ili kuthibitisha kuwa maisha ambayo Yesu aliyaishi, alikuwa akiyaishi kwa ajili ya kila mmoja wetu. Ilikuwa ni kana kwamba tulikuwa ndani Yake, tukiteseka pamoja Naye. Kwa hivyo, Paulo anamalizia akisema hivi: “tupate na kutukuzwa pamoja naye.”

Fikiria pia kitabu cha Warumi 6:4.

> "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima." Warumi 6:4

Paulo anazungumzia wakati uliopo. Yesu alizikwa miaka elfu mbili iliyopita, ila Paulo anazungumza kana kwamba tulikuwa ndani Yake wakati hili ilipotokea. Njia pekee ambayo dhabihu ya Kristo inaweza kukubaliwa kisheria ni kama ikiwa ni ya kujitoa sadaka; ikiwa ni kwa niaba yetu. Hivyo ndivyo kuhani mkuu alivyokuwa akiwakilisha alipoyabeba moyoni mwake majina ya makabila kumi na mawili ya Israeli. Tunateseka pamoja na Kristo, na tumezikwa pamoja na Kristo. Sasa tazama mstari wa 8.

> “Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye;” Warumi 6:8

Hakika Kristo hajafa. Kwenye mstari huu, Paulo anadhihirisha kifo cha utu wa kale kwenye ubatizo. Anasema kuwa endapo tutakufa pamoja na Kristo kwenye maji ya ubatizo, “pia tutaishi pamoja naye”. Mitume waliyaelezea maisha ya Kristo, kifo, mateso na ufufuko wake katika wakati uliopo ili kudhihirisha kwamba tulikuwa pamoja naye, tukipitia njia yake hiyo hiyo.

> "Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu." Wakolosai 2:12

“Utendaji kazi wa Mungu” unaozungumziwa kwenye mstari huu ni

uweza wa Roho Mtakatifu; utukufu wa Baba aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu. Yeyote ambaye—kwa imani—amezikwa pamoja na Kristo kwenye ubatizo anafufuliwa kwa nguvu ile ile; utukufu wa Baba. Ni utendaji kazi wa Mungu. Kwa mara nyingine tena Paulo anatuonyesha kwamba tumezikwa na kufufuka pamoja na Kristo wakati huu wa sasa.

> "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu." Wakolosai 3:1

Katika kitabu cha Wakolosai 3:1, msalaba unakuwa jambo la sasa kwa Mkristo. Hii ndiyo jambo waandishi wa agano la kwanza waliendelea kusisitiza. Hatupaswi kutazama msalaba kama jambo iliyotokea miaka elf mbili iliyopita, lakini kama tukio inayofanyika katika maisha zetu kila wakati. Wakati mkisto anapotubu kwa hakika, kujisalimisha, na kutafuta msamaha, watapitia hali Kristo aliyopitia. Watakufia dhambi, na kufufuka naye kwa maisha mapya naye. Msalaba unakuwa ni kitu cha wakati huu wa sasa kwao. Hata hivyo Kristo alikuwa akifanya hivyo kwa niaba yao miaka elfu mbili hapo kabla.

> "Kristo atakapofufuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafufuliwa pamoja naye katika utukufu." Wakolosai 3:4

Linganisha huu mstari, Wakolosai 3:4 na andiko lifuatalo kwenye kitabu cha Waebrania 9:28.

> “Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.” Waebrania 9:28

Mistari hizi inasema ukweli mkuu: Maisha ya Kristo inakuwa ni yetu. Ni kwa sababu hii wakati mtume Paulo alipokuwa akifundisha haki kwa imani, angesema hivi:

> "Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki." Warumi 4:5

Kwa nini imani ya aaminiye inahesabiwa kuwa ni haki? Ni kwa sababu mara tu unapomuamini Yesu, maisha Yake yote yanawekwa kwako. Kama vile Yesu anavyobeba jina lako mbele za Baba, Baba haoni mtu mwingine ila yule mtakatifu na asiye na unajisi; Kuhani Mkuu. Hiyo tu ndiyo anaona. Na jina lako lipo kifuani Mwake. Matokeo yake ni kwamba, Baba anaona haki kamilifu ya Mwanawe ndani yako. Ndiyo maana tunasoma kwamba "kwa moyo mtu huamini hata kupata haki". Warumi 10:10. Si kwa sababu ya kile ambacho mtu anafanya bali ni kile anaamini.

Unapomkubali Kristo kwa imani, unapokea uzima wake. Unapokea utiifu Wake, haki Yake, kifo Chake, ufufuo Wake, na kwenye ufufuo wa kwanza, kutukuzwa Kwake. Ndiyo maana Paulo anasema "uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu." Wakolosai 3:3. Maisha yako hayaonekani tena. Ni maisha yaliyo kamilifu ya Kristo aliyoishi kwa niaba yako ambayo Baba anaona kwenye hukumu. Kristo amebeba jina lako ndani ya moyo Wake na upatanisho unafanywa. Ndio maana mtume anasema "ametuneemesha katika huyo Mpendwa". Waefeso 1:6.

Njia pekee ambayo hii inaweza kuwa halali ni kama kila kitu ambacho Yesu alikifanya kwenye maisha yake yote (na sio tu pale msalabani) kilifanywa kwa niaba ya wanadamu wote. Hii ni muhimu kwa sababu ikiwa ni msalaba peke yake unaoleta msamaha wa dhambi, Yesu angekuja duniani akiwa mtu mzima, akaishi siku moja au mbili, akafa msalabani, na kurudi juu mbinguni. Angezilipia dhambi zetu, lakini je, hiyo peke yake ingetosha? Hapana. Maisha yake yote yalipaswa kuwa ni dhabihu. Msalaba ulikuwa ni kilele tu cha kila kitu Alichokifanya kwenye maisha Yake yote. Kujitoa kama sadaka isingetosha. Alikuwa anatuwakilisha kila wakati Alipokuwa hapa duniani. Ndiyo maana inaitwa kujitoa sadaka. Kamusi ya *Merriam-Webster* inafafanua kujitoa sadaka kama hivi:

> 2: kufanywa au kuteswa kwa niaba ya mtu mwingine au kwa manufaa ya mtu mwingine: mbadala <kujitoa sadaka>

Kwa mwangaza wa ufafanuzi huu, mzazi yeyote mwenye upendo

ambaye hutoa dhabihu kubwa kwa ajili ya watoto wake anaishi kwa kujitoa sadaka. Yeyote anayejitolea kwenye shida na kujikana, labda kwenye vita au umaskini, anaishi kwa kujitoa sadaka. Ni upendo ambao "hautafuti mambo yake". Kitabu cha 1 Wakorintho 13:5. Ni upendo wa kujitolea; tabia hasa ya Mungu inayojitokeza moyoni mwa mtu.

Walakini hii haina uhusiano wowote na masharti ya kisheria. Mtu hafanyi kitu kizuri kwa mtu mwingine kwa sababu ni jambo sahihi kulifanya, lakini kwa sababu ni suala la kiasili. Ni kanuni. Maisha ya mtoto ni sehemu ya maisha ya mzazi. Mtoto anapoteseka, mzazi huumia. Mtoto anapofurahia, mzazi anafurahia. Maisha yao yameunganishwa. Kwa hiyo mzazi akimuona mtoto wake akiwa kwenye matatizo, haachi kutafakari anachopaswa kukifanya. Anatenda tu moja kwa moja bila kusita. Ni suala la kiasili. Hiyo ndiyo maana ya kuishi kwa kujitoa sadaka. Na hivi ndivyo Kristo alivyoishi maisha Yake yote hapa Duniani. Ilikuwa ni msukumo wa kiasili Kwake kuishi na kuwasaidia wengine.

Hakika, Mungu ametujalia upendo huu ili tuweze kumuelewa vyema, tabia yake, na upendo wake kwetu. Pale mtu unayempenda anapoteseka, hauwezi kufurahia maisha. Haiwezekani. Baba na Mwana hawangeweza kufurahia amani ya mbinguni huku mambo yakiwa mabaya duniani. Haiwezekani kwa sababu Mungu ni pendo.

Nilibahatika kulelewa kwenye nyumba ambayo nilijionea upendo huu wa kujitoa sadaka. Siku chache tu kabla ya mama yangu kufa, alikuwa amelazwa kwenye kitanda cha hospitalini akiwa na kiunzi cha mifupa, na maneno ya mwisho kabisa aliyoniambia yalikuwa ni haya: “Bill, umekula?” Maisha yote ya mama yangu, tangu kuzaa watoto hadi kufa kwake, yalikuwa ni kwa ajili ya watoto wake. Utafikiri kwamba endapo mtu anakufa, mawazo yake yatakuwa juu yake yeye mwenyewe, na juu ya kile kitakachompata. Kwa mama yangu, bado ilikuwa ni suala la kuwajali watoto wake. Kutuweka mbele mimi na ndugu zangu ilikuwa ni kawaida kwake.

Kwa upendo wa aina hii utatoa sadaka yoyote kwa mpendwa. Ndio maana wazazi hujitolea kwa ajili ya watoto wao. Yesu mwenyewe alisema: “Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai

wake kwa ajili ya rafiki zake." Yohana 15:13.

Mstari hii inanikumbusha hadithi kwenye Agano la Kale. Wakati fulani, Mungu alitaka kuiangamiza Israeli yote haraka kutokana na uasi wao. Lakini Musa akamgeukia Mungu wa mbinguni na kusema: "Ughairi uovu huu ulionao juu ya watu wako." Kutoka 32:12.

Inashangaza sana! Aya hii inastahili kutafakariwa sana na kwa kina. Hapa, mwanadamu anayeweza kufa anazungumza na Muumba wa ulimwengu, na anamuambia Mungu aghairi. Lakini Musa anazungumza kutokana na upendo wa dhati kwa Israeli kiasi kwamba Mungu anaruhusu mazungumzo yatokee. Kwa hakika, ni Kristo Mwenyewe ndiye aliyekuwa akihimiza na kuzungumza kupitia kwa Musa. Musa alikuwa akijifananisha na watu wa Israeli, hata akaona ni afadhali aangamie yeye kuliko kuwaona wao wamepotea. Hakuwaacha waende zao. Hivyo ndivyo Yesu alivyo. Kristo asingeweza kubakia mbinguni huku Akituona sisi tukiangamia duniani. Badala yake, wakati Adamu alipotenda dhambi, Kristo alisema hivi: "Adhabu iniangukie; nitasimama mahali pa mwanadamu. Atapata nafasi nyingine." {FLB 75.3} Kristo alipotoa ahadi hiyo, ilikuwa ni kwa niaba ya wanadamu wote, si kwa wale waliookolewa tu. Na kama Kristo angeshindwa, basi binadamu wote wangepotea. Lakini kama Angefaulu, basi binadamu wote wangeweza kuokolewa. Hakuna wa kupotea. Yesu alijitoa sadaka kwa ajili ya watu Wake. Aliishi maisha Yake yote kama sadaka ya kujitolea kwa ajili ya manufaa ya wengine. Kuna aya nyingi sana juu ya jambo hili lakini hapa chini ni baadhi ya chache tu.

> "...mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa [yetu]." Mt 8:17

> "Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu…" Isaya 53:4

> "Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona." Isaya 53:5

"ila twamwona yeye… kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu." Waebrania 2:9

“Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti…” 1 Petro 2:24

“Adhabu Iniangukie Mimi. Nitasimama mahali pa mwanadamu. Atapata nafasi nyingine.” {FLB 75.3}

Kristo alipotoa ahadi hiyo, aliunganisha nafsi yake na sisi na hawezi kujiondoa kwenye huo muungano. Hivyo ndivyo aya ifuatayo inavyosema.

“yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho.” 2 Wakorintho 5:19

Kristo atawezaje kukupatanisha endapo haujazaliwa mara ya pili? Wakati huo (msalaba) bado kuna miaka elfu mbili ijayo ya historia. Hata hivyo mstari huu unasema kwamba mlipatanishwa msalabani. Upatanisho ulifanyika kwa kila mwanadamu, na kuwapa nafasi ya wokovu.

Hii inawezaje kuwa hivyo? Jibu ni kuwa uliwakilishwa ndani ya Yesu pale msalabani. Ndivyo tulivyoona hapo awali kwenye orodha za aya zilizopita. Na hivyo ndivyo Alivyoweza kuupatanisha ulimwengu na nafsi Yake, wakati uliopita na wakati ujao. Kila jambo ambalo Kristo alifanya ilikuwa ni kwa niaba yetu. Alibeba majukumu kwa jamii nzima ya wanadamu. Alimpulizia Adamu pumzi ya uhai na kuchukua jukumu kwenye uzao wa Adamu. Hiyo ni sehemu ya agano la milele alilofanya na Baba yake. Kwangu, njia rahisi zaidi ya kuyafupisha maagano haya mawili ni hii. Kwenye Agano la Kale kwenye Mlima Sinai, Israeli waliahidiwa hivi: “Hayo yote aliyoyasema BWANA tutayatenda.” Kutoka 19:8. Na maneno yao wenyewe ndiyo yaliyowafanya washindwe. Walifikiri kwamba kwa nguvu zao wenyewe wangeweza kumtii Mungu. Kwa agano la milele, au agano jipya, Kristo ameahidi kutii kwa niaba yetu. Mkristo huweka imani yake Kwake na anaishi maisha Yake makamilifu ndani yao. Agano la kwanza lilikuwa ni agano la kazi ambalo lil-

ishindikana, kwa sababu mwanadamu peke yake atashindwa daima. La pili imebuniwa kwa Kristo ambaye aliishi, akafa na kufufuka kwa niaba yetu na ambaye Huyatoa maisha yake makamilifu ya utii kwa kila mmoja wetu. Fikiria maandiko haya mazuri ambayo yanaangazia jambo hili:

"… **tumepewa** mtoto mwanamume…" Isaya 9:6

"...BWANA ameweka juu yake Maovu **yetu sisi** sote." Isaya 53:6

"Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao." Mathayo 1:21

"alimfanya [kuwa] dhambi kwa ajili **yetu**…" 2 Wakorintho 5:21

"Kristo alitukomboa **katika** laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili **yetu**..." Wagalatia 3:13

## SURA YA 3

Mada hii ya ajabu ya Kristo anayetuwakilisha inajirudia rudia kwenye Biblia yote. Kwa kuzingatia maandiko yaliyotangulia, zingatia kauli ifuatayo kutoka kwenye *The Desire of Ages*.

> "Kwa niaba ya mwanadamu, Kristo alishinda kwa kuvumilia jaribu kali zaidi. Kwa ajili yetu Alitumia uwezo wa kujidhibiti wenye nguvu kuliko njaa au kifo. Na kwenye ushindi huu wa kwanza yalihusika masuala mengine ambayo yanaingia kwenye migogoro yetu yote na nguvu za giza." {DA 117.4}

Kama nukuu hii inavyoangazia, kifo cha Kristo msalabani pekee kisingetosha. Malipo ya dhambi zako pekee hayatoshi. Ilimbidi Yesu atuletee maisha na uwezo ambayo ingetuwezesha kupata ushindi juu ya migogoro yetu na Shetani. Ni zaidi ya kulipia dhambi zako tu; ni nguvu ya kukuokoa na dhambi zako ambayo ni ya muhimu sana. Kutoka kwenye *The Review and Herald*, tunasoma hivi:

> "Mtazame Mwokozi wetu wa thamani akiteseka nyikani, akiinama chini ya mzigo wa hatia ya mwanadamu, na kustahimili maumivu makali ya njaa… alikuwa Mtoto wa Mfalme wa mbinguni; bali kwa ajili ya wanadamu akafanyika dhambi kwa ajili ya wahusika wote."
> {RH, Septemba 23, 1890 kifungu cha 3}

Baada ya kusoma nukuu hii, nilipata mtazamo mpya juu ya mateso ya Kristo. Nilijua kuwa pale msalabani Yesu alizipokea dhambi na hatia zetu. Lakini kauli hii inaelekeza mwanzoni mwa huduma Yake, mara tu baada ya ubatizo Wake. Ni wakati huu ambapo anamuelezea Yesu kama "akihisi mzigo wa dhambi na hatia ya mwanadamu". Ni wakati huu ambapo dada White anasema hivi: "kwa ajili ya wanadamu akafanyika dhambi kwa ajili ya wahusika". Mara tu Kristo alipochukua jukumu la kutuokoa, basi hatia, matatizo, na kukosa tumaini vilikuwa vikisumbua nafsi Yake.

> "Amebeba kila jaribu lililowekwa juu yake. Hakushindwa kwenye jangwa la majaribu alipovumilia shinikizo la hatia ya Adamu na ile

> ya uzao wake.” {3SP ukurasa wa 38}

Kristo alikuwa akiishi na kuteseka kwa ajili yetu muda mrefu kabla ya pale Kalvari. Fikiria taarifa nyingine ya kuvutia:

> Kubebwa kwa Ugonjwa wa Wengine kwa Kujitoa Sadaka
>
> “Kristo peke yake ndiye aliyeweza kustahimili mateso ya wanadamu wote. "Aliteswa kwenye dhiki zao zote." Hakuwahi kuwa na ugonjwa kwenye mwili Wake, bali Alibeba magonjwa ya watu wengine. Wakati wanadamu wanaoteseka walipomsongea Yeye, Yeye aliyekuwa kwenye afya ya utu uzima uliokamilika alikuwa ni kama aliyeteswa pamoja nao...” {3SM 133.2}

Tunawezaje kuelewa kuwa Kristo “alibeba magonjwa ya watu wengine” na bado siku zote hakuwa na ugonjwa? Ni kwa kuelewa tu uhusiano uliopo kati ya mzazi na mtoto. Mtoto anapougua, mzazi yeye mwenyewe anaweza pia kuwa na ugonjwa huo. Kwa njia nyingi, hii inaweza kumuumiza zaidi mzazi kuliko mtoto. Hicho ndicho Sister White anachokizungumzia.

Ule ukweli tu kuwa Mungu alimuumba mwanadamu kwa sura na mfano wake hutuambia mengi kuhusu jinsi Anavyotutazama, na jinsi Anavyoteseka kutuona tunamkana au kutomtii. Kauli hii ni ukweli kwa sasa. Ingawa Mtoto wa Mungu yupo mbinguni, sasa anateseka sana kama vile alipokuwa duniani.

Yesu Alijitambulisha kuwa ni mmoja wetu kwa kila njia. Aliteseka pamoja nasi; akapatwa na huzuni pamoja nasi; alifahamu huzuni na hatia zetu, na Aliubeba mzigo huu mpaka msalabani. Tazama kauli inayofuatia.

> “Aliogopa kuwa dhambi ilikuwa ni chukizo sana kwa Mungu kiasi kwamba wangetengana milele. Kristo aliuhisi uchungu ambao mwenye dhambi ataupata wakati rehema isipomuombea tena mtu mwenye hatia.” {DA 753}

Unafikiri uchungu huo ilimaanisha nini? Huo ndio uchungu wa kupotea; wakati rehema isipokuweko kwa ajili ya mwanadamu tena. Hivyo ndivyo Kristo alivyohisi akiwa pale msalabani. Kwa maneno mengine, Yeye hakuwa tu akifa kifo cha kwanza. Kile ambacho Yesu alikuwa akikipitia kwa niaba ya wanadamu kilikuwa ni kifo cha mtenda dhambi asiyetubu. Kristo alikuwa akishuhudia kifo cha milele; kifo cha pili. Kwa maana "Aliogopa kuwa dhambi ilikuwa ni chukizo sana kwa Mungu kiasi kwamba wangetengana milele."

Uthibitisho wa Biblia unaeleza kwa hekima kuwa "kwa mtu anayeamini, kifo ni jambo dogo tu." {DA 787}. Shetani amekitukuza kifo, na bado kwa Mkristo hakizai uchungu. Kwa njia nyingi, kifo ni furaha kwa sababu hakuna mateso tena, na muamini hufa na tumaini hilo zuri lenye baraka. Wanajua kwamba kifo chao kitaonekana kuwa ni kufumba na kufumbua tu, na wataamka ili kumuona Mwokozi wao akirudi kuwalaki kwenye mawingu. Ni jambo zuri. Lakini hicho sicho kifo ambacho Sister White anakielezea kwamba Yesu anakufa nacho. Kristo aliuhisi uchungu wa kupotea milele, ambao ni mshahara wa dhambi (Warumi 6:23).

> "Hakua na hatia wala kustahili adhabu, Mbadala wetu na Mdhamini wetu alileTwa chini ya laana na hukumu ambayo ingepaswa kuwa yetu." {ST Desemba 8, 1898}

Je, ni laana na hukumu gani ambayo ingekuwa kwetu? Ni kifo ya milele. Hiyo ndiyo Kristo aliweka chini yake. Hicho ndicho Alichoadhibiwa kama mwakilishi wa jamii iliyoanguka; yaani, wewe na mimi.

> "Ni lazima ashuke kutoka kwenye usafi na amani ya mbinguni, furaha na utukufu wake na uzima wa kutokufa, na kukutana na uharibifu wa dunia, ili kustahimili huzuni, aibu, na kifo chake. Alitakiwa kusimama kati ya mwenye dhambi na adhabu ya dhambi…" {PP 64}

Mshahara wa dhambi ni mauti ya milele. Na Yesu alipaswa kuipata adhabu hiyo juu Yake Yeye Mwenyewe.

> “Adhabu ya uvunjaji wa sheria ya Mungu ni kifo. Kristo aliteseka kwenye mauti kwa ajili ya mwanadamu, na kuuleta uzima na kutokufa kwenye nuru kutoka kwa wafu.” {RH Machi 9, 1886}

Tunajua kuwa kila mtu anafufuliwa kutoka kwenye kifo cha kwanza kwa sababu ni usingizi tu. Kwa hivyo, kinachozungumziwa hapa ni kutoweka milele. Uvunjaji wa sheria ya Mungu—mshahara wa dhambi—ni kifo ya milele. Na hiyo ndiyo kifo ambayo Kristo aliteseka nayo. Yeye Aliichukua adhabu hiyo Kwake. Hata hivyo Kristo alishinda hukumu hiyo kwa kufufuka kutoka kwa wafu, na hivyo kuleta uzima na kutokufa kwenye nuru.

> “Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.” [Warumi 6:23.]…Kifo kinachoelezewa kwenye maandiko haya si kile kilichotamkwa juu ya Adamu, kwa maana wanadamu wote wanakabiliwa na adhabu ya kosa lake. Ni “kifo cha pili” ambayo ni tofauti na uzima wa milele. {GC88 544.1}

Kristo alipatwa na mauti ya pili. Ndiyo maana Hakuweza kuona kupitia milango ya kaburini. Ndiyo maana tumaini halikujidhihirisha ndani Yake akitokea kama mshindi. Alihisi kujitenga kwake na Mungu kungekuwa ni ya milele. Kristo alikuwa akifa kwa hatma ya mwenye dhambi na kupokea adhabu ya mtenda dhambi kwa ajili ya mshahara wa dhambi.

Tunapoelewa hii kwa undani, tunajua kuwa hatupo chini ya hukumu tena. Kwa nini? Kwa sababu Yesu aliichukua hukumu. Hatupaswi kuwa na hatia tena. Kwa imani unapokubali maisha ya Kristo kuwa yako—mateso Yake, utiifu, kifo na ufufuo wake—basi unakubali haki Yake, na Mungu anakuhesabia haki ya Mwanawe.

Lakini unapaswa kuamini. Unapaswa kuhesabu kuwa maisha yako ya zamani yalikufa pamoja Naye kama Paulo anavyosema. Sio dhambi zako tu bali ni maisha yako yote ambayo ni lazima yafe pamoja Naye. Unapaswa kuamini kuwa Yesu alijitwika dhambi zako, hatia na hukumu. Yote ni sehemu ya kuamini kwa imani unapoungama dhambi zako

na kumuamini Kristo. Zisiwe ni porojo tu. Ina maana kuwa unaamini kweli maisha yako ya zamani imeuawa na kuharibiwa.

Kumbuka kwamba ubinadamu uliotukuzwa ndiyo ilitoka kaburini. Kwa hivyo ni nini ilifanyikia maisha ambayo yalipata laana ya dhambi pale msalabani? Ilibakia kaburini.

> "Kristo alisulubishwa… Alikuwa amelala kwenye kaburi jipya la Yusufu. Kristo alishuka kaburini kama Mchukua dhambi wetu, akilifungua kaburi la dhambi za wote ambao watamkubali kama Mwokozi wao binafsi." {12MR 411.1}

Ni muhimu sana kuelewa jambo hili. Uthibitisho wa Biblia unamaanisha nini unaposema "Kristo alishuka kaburini kama Mchukua dhambi wetu, akilifungua kaburi la dhambi za wote ambao watamkubali kama Mwokozi wao binafsi"?

Pale msalabani, Yesu alikuwa amebeba dhambi ya ulimwengu. Kwenye kitabu cha Isaya 53:6 tunasoma hivi: "…BWANA ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote." Mtume Petro anaandika kuwa: "Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti". 1 Petro 2:24

Sister White anabainisha kuwa Kristo alizichukua dhambi hizo kutoka msalabani mpaka kaburini. "Kristo alishuka kaburini kama mchukua dhambi wetu". {12MR 411} Lakini pia anasema wazi kuwa "Kristo alitoka kaburini akiwa ametukuzwa" {DA 780} na hapakuwa na alama za dhambi juu Yake. Basi ni nini ilifanyikia dhambi zetu?

Nusu ya pili ya kauli hiyo inatoa jibu. Kristo alifungua "kaburi la dhambi za wote ambao watamkubali".

Ndiyo maana Paulo anasema kuwa tumezikwa pamoja na Kristo kwenye ubatizo, na pia kufufuka pamoja Naye. Kristo alilifungua kaburi kwa ajili ya dhambi za wote ambao watamkubali. Hii ni zaidi ya msamaha tu. Maisha yako ya zamani yanatakiwa kuzikwa kabisa pale msalabani. Kwa imani inakupasa kuamini kwamba utu wa kale ulisulubishwa pale pamoja Naye. Kwa kuzingatia hili, Paulo anasema kuwa:

> “Maana, upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote;” 2 Wakorintho 5:14

Kristo alifungua kaburi kwa ajili ya dhambi za wote ambao watamkubali. Kwa hiyo, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya wote, unaweza kuamini kuwa ulikufa pamoja naye pale msalabani. Je, hii ina maana gani kwenye matendo? Tazama huu mstari ufuatao.

> "tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao." 2 Wakorintho 5:15

Wale wanaoishi “wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe” kwa sababu utu wa kale haupo hai tena. Kama Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, unashiriki upya wa maisha. Unatoka kaburini, lile kaburi lililojaa maji (ubatizo), kama mtu mpya kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu.

Kumbuka maneno ya mwanzo ya Paulo kwenye kitabu cha 2 Wakorintho 5:14: “Maana, upendo wa Kristo watubidisha”. Tuliona kuwa ni jambo la kawaida kwa mzazi kujitolea kwa ajili ya mtoto wake. Unapotafakari kile ambacho Yesu alikufanyia kwenye maisha Yake yote na kuelewa upendo Wake, hiyo itakulazimisha na kukushurutisha kutoa dhabihu kwa ajili Yake. Kwa sababu ya upendo wa Kristo ndani yako, hautataka kufanya jambo lolote lingine ila tu kuishi kwa ajili Yake Yeye aliyekufa kwa ajili yako.

Kwa maneno mengine, upendo huzaa upendo. Je, kama ukimkosea mtu, unapokea malipo ya upendo? Hapana; unapokea kutoaminiwa na ikiwezekana hata kukasirikiwa na kuchukiwa. Kwa kanuni hiyo hiyo, unapofanya jambo la haki na kuonesha upendo kwa mtu, unapokea malipo ya upendo. Unapokea uaminifu, shukrani na kujitolea. Unapopokea upendo wa Kristo kama Paulo anavyoeleza hapa, utataka kumtumikia na kuishi kwa ajili Yake. Utarudisha upendo ulioonyeshwa. Na kanuni hii inapotawala matendo yako—kama inavyofanya kwa mzazi mwenye upendo—haitakuwa vigumu kuishi kwa ajili ya Kristo. Haitakuwa vigumu kuacha dhambi yoyote inayokusumbua kwenye

maisha yako kwa sababu kuna jambo lenye nguvu zaidi linalokupa hamasa. Angalia kile ambacho Petro anakisema:

> "Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa." 1 Petro 2:24

Umeshawahi kujiuliza ni kwa nini mitume waliunganisha tena na tena kifo chetu kwa dhambi na kifo cha Kristo pale mtini? Jibu ni kwa sababu tulikuwa ndani Yake wakati Alipokufa. Yesu hakuwa mbadala pekee; Aliishi kwa urahisi kama sehemu yetu. Kila tendo baya tulilolifanya, kila fikra mbaya na hatia yote inayoletwa iliwekwa juu Yake. Na kwa kupigwa kwake—kwa ufahamu wa maisha Yake ya mateso kwa ajili yetu—tutaponywa, na kuongozwa na upendo wa kuishi kwa ajili Yake. Unapoamini kweli kuwa umesulubishwa pamoja na Kristo, utaamini kuwa umekufa kwa ajili ya dhambi kama vile Petro anasema. Utaamini kuwa Yesu alifungua kaburi sio tu kwa ajili ya dhambi zako bali kwa ajili ya ule utu wa kale uliotenda dhambi hizo.

Haitoshi kwa Yesu kufa kwa ajili ya dhambi zako tu, kwa sababu utu wa kale utaendelea kutenda dhambi. Huo utu wa kale hauna budi kusulubiwa pamoja Naye, na kuachwa pale kaburini. Sheria ya dhambi ilihukumiwa kwenye mwili Wake mwenyewe pale mtini. Ni kwa uwezo huu ndipo unapoweza kuishi kwenye haki. Ndiyo maana mitume anaandika hivi: “ambaye kwa kupigwa kwake mliponywa”.

Kwenye kitabu cha Isaya 53, Isaya anatazamia mbele kwenye unabii na anasema wazi kuwa “kwa kupigwa kwake sisi tumepona.” Kwenye kitabu cha 1 Petro 2, Petro anatazama nyuma kwenye msalaba na kusema hivi: "kwa kupigwa kwake mliponywa". Wale mitume walielewa nguvu ambayo ilidhihirishwa pale msalabani. Walielewa kuwa hapo ndipo waliponywa.

> “Kristo alijitoa kwa kila kitu kwa ajili ya mwanadamu ili atengeneze njia ambayo ingewezekana kwa mwanadamu kuifikia mbingu. Sasa ni jukumu la mwanadamu kuonyesha kile atatoa kwa matendo yake mwenyewe kwa ajili ya Kristo, ili apate utukufu usio na

> mauti." {RH, Septemba 23, 1890}

Tunaposoma mada ya injili na maisha ya Kristo ya mateso kwa ajili yetu; tunapoona ni kiasi gani Alijitoa kwa ajili yetu, tunaweza kusema pamoja na Paulo kuwa upendo wa Kristo unatusukuma, "maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote: Na [ya kuwa] alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao." Kama ambavyo Petro anasema, tunatakiwa kuishi kwa haki. "Sasa ni kwa mwanadamu ambaye ameanguka kuonyesha kile ambacho atakitoa kwa matendo yake mwenyewe kwa ajili ya Kristo, ili aupate utukufu usio na mauti." {3T 481}

Ingawa ukweli huu ni mzuri, bado unatambulika tu kwenye mioyo ya watu wachache.

> "Wachache, ndiyo, wachache tu, kwenye idadi kubwa sana ya watu duniani wataokolewa kwenye uzima wa milele, huku umati ambao haujaziweka sawa nafsi zao kwe kutii ukweli watawekwa kwenye kifo cha pili. Wakati dhambi za wanaoamini waliotubu zikiondolewa mahali patakatifu, kutakuwa na kazi ya pekee ya utakaso, ya kuondoa dhambi miongoni mwa watu wa Mungu huku duniani." {FLB 213}

Hapo ndipo tulipoanzia kwenye kitabu cha Waebrania 9:28, na hapo ndipo inapoishia. Cha kusikitisha ni kuwa, ni wachache tu miongoni mwa idadi kubwa ya watu ambao wapo tayari kukubali yale ambayo Yesu Kristo amewafanyia na bado anayafanya mpaka hivi leo.

## SURA YA 4

> "Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu." Waebrania 9:28

Tumekuwa tukijifunza kifungu hiki cha kustaajabisha tukilenga kwenye mwanga wa maisha ya kujitoa sadaka ya Kristo, kifo, na ufufuo kwa niaba yetu. Kwenye hii sura, tutaona namna ambavyo ubatizo unafanya hili jambo liwe ni kitu binafsi na cha kuonekana maishani.

Kitabu cha Waebrania 9:28 kinaweka mkazo kwenye siku isiyo ya kawaida ya upatanisho na utakaso wa dhambi kutokea mahali patakatifu pa mbinguni. Hatimaye, kumbukumbu ya dhambi itakaposafishwa kutoka mahali patakatifu, Yesu atarudi "pasipo dhambi" kuleta wokovu kwa wale ambao wamekuwa wakimtafuta. Kwenye hatua hii, Yesu anasema hivi: "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa." Ufunuo 22:11. Mistari hii miwili (Waebrania 9:28 na Ufunuo 22:11) inatufundisha kuwa kila mmoja wetu anakabiliwa na hukumu ya wakati ujao, na kuwa hatima yetu imetiwa muhuri juu ya kifo chetu cha hapa duniani, au endapo bado tupo hai, wakati pale Bwana atakaporudi.

Licha ya hayo, makanisa yanadanganya kuwa dhambi zetu zilifutwa pale msalabani. Kwa sehemu kubwa, Ukristo wa kisasa unafundisha kuwa tulihukumiwa na kuokolewa pale msalabani. Na kwa vile msalaba unawakilisha ubatizo wa mtu na uamuzi kwa ajili ya Kristo, mara nyingi Wakristo wengi hutaja siku yao ya ubatizo kuwa ndio siku ambayo waliokolewa.

Kutokana na kosa hili la msingi linaibuka fundisho la uongo: 'ukishaokolewa, basi umeokolewa daima'. Mafundisho haya yanaondoa kabisa hitaji la hukumu ya mwisho au ya siku zijazo, pamoja na hitaji la mahali patakatifu pa mbinguni. Kwa maana kama mtu alihukumiwa na kuokolewa milele pale msalabani, kungekuwa na haja gani hii leo Kuhani Mkuu kutoa huduma mahali patakatifu pa mbinguni? Au

kungekuwa na haja gani ya mahali patakatifu kutakaswa dhambi kabla Kristo hajarejea?

Inashangaza sana, ukweli huu ulio wazi na ambao ni rahisi kuhusu mahali patakatifu pa mbinguni ni wa kipekee kwa Kanisa la Waadventista Wasabato. Hata hivyo, ushindi kamili juu ya dhambi hauaminiwi au kufundishwa hata kwenye Mkutano wa Kanisa la SDA.

Ngoja nikupatie kielelezo. Mwenye dhambi anasikia injili mnamo mwaka 2015. Anatubu kweli na kupokea msamaha. Anabatizwa na hivyo kuamini kuwa amepokea wokovu. Baada ya kubatizwa, mtu huyo hatendi sana dhambi, lakini bado anatenda dhambi. Mnamo mwaka 2018, mtu huyo anafariki.

Kwa aina hii ya injili, ni nini ambacho msalaba umekifanikisha? Hakuna. Mtu huyo alikuwa akitenda dhambi kabla ya ubatizo wake, na bado anafanya dhambi baada ya huo ubatizo wake. Kwa hakika, kielelezo hiki kinaelezea mafundisho ya kiinjili ya kuokolewa na kuhukumiwa msalabani au 'ukishaokolewa, basi umeokolewa daima'. Kwa bahati mbaya, mafundisho haya yamekuwa ni theolojia mpya ya Mkutano wa Kanisa la Waadventista Wasabato na wakristo wa makanisa zingine.

Kwa miaka mingi, Shetani amekuwa akifanya kazi ya kuuharibu ujumbe wa mahali patakatifu—kwanza kwa kupitia Ballinger enzi za Sister White, na kisha kupitia kwa Desmond Ford na wengineo wengi—kwenye jitihada za kuuharibu utakaso wa rekodi ya dhambi kwenye maisha ya mtu.

Kinachoshangaza ni kuwa wale wanaoshikilia theolojia hii mpya wanafanya hivyo kwa sababu wanadai kuwa wanaishi chini ya agano jipya. Katika hali halisi, hii theolojia mpya ni sawa kabisa na ile iliyotekelezwa chini ya mfumo wa agano la kale! Kwa mfano, kwenye agano la kale, mwenye dhambi angepeleka mwanakondoo mahali patakatifu, kuungama dhambi zake juu ya dhabihu hiyo na kisha kurejea nyumbani. Wakati mwingine alipotenda dhambi angetoa dhabihu tena, na hii ingerudiwa mara kwa mara kwa sababu dhambi iko ndani yake, asingeweza kuacha kutenda dhambi. Hiyo dhabihu ilikuwa inaende-

leza dhambi. Fikiria kile ambacho Paulo anakisema kuhusu mfumo wa agano la kale.

> “Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wowote kuwakamilisha wakaribiao.
>
> Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?
>
> Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi." Waebrania 10:1, 2, 11

Paulo anasema kuwa agano jipya lilipaswa kuchukua nafasi ya lile agano la kale, ambalo lilikuwa limepitwa na wakati na kutokuwa hai tena.

> “Kwa kule kusema, Agano jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu kutoweka.” Waebrania 8:13

Agano la kale halikuwa likitimiza kusudi la Mungu kwa watu Wake. Walakini, hakukuwa na kosa kwenye agano lenyewe. Kumbuka kuwa Kristo mwenyewe aliishi chini ya agano la kale na bado Hakutenda dhambi. Kwenye kitabu cha Waebrania 8:8, Paulo anaeleza waziwazi sehemu ilipokuwa na kosa kwenye agano la kale.

> “Maana, awalaumupo, asema
>
> Angalia, siku zinakuja, asema Bwana,
>
> Nami nitawatimizia nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda agano jipya;” Waebrania 8:8

Tatizo kwa agano la kale ilikuwa ni watu. “Hayo yote aliyoyasema BWA-

NA tutayatenda," ilikuwa usemi wao. Kwenye kitabu cha Kutoka 19:8. Watu walikuwa wamedhamiria kumtii Mungu kwa kutumia nguvu zao wenyewe, na hapo wakaanguka wenyewe. Njia hii haikuweza kumkamilisha mhitaji wa msamaha na kwa hakika haikuweza kumzuia yeye kutenda dhambi.

Leo hii msalaba unatazamwa vivyo hivyo. Kumbuka mfano wetu wa mtu mwenye dhambi. Mara tu anaposikia injili, anatubu kweli, kuungama dhambi zake na kuamini kuwa ameokoka. Baada ya kuukubali msalaba, hasemi uongo wala hafanyi tena uzinzi, na maisha yake hakika yamekuwa ni bora. Anaweza hata kuwa mfadhili na kutumia sehemu kubwa ya maisha yake kuwatumikia watu wengine. Hata hivyo, mielekeo ya ubinafsi bado inafanywa; dhambi haijasitishwa kabisa. Kisha siku moja anafariki. Wainjilisti wanaamini kuwa ameokoka kwa sababu dhambi zake zililipiwa mara ya kwanza wakati alipoukubali ujumbe. Hawazingatii kuwa maisha yake bado yalitawaliwa na ubinafsi; utu wake wa kale haujafa. Aliboresha tu baadhi ya sehemu za maisha yake.

Wakristo wengi sana wanaangukia kwenye kundi hili. Bila kujali dhehebu la mtu, kama bado kuna dhambi kwenye maisha ya mtu, nafsi ina mamlaka ya kutawala. Huenda mtu ameacha dhambi kubwa, lakini bado kuna kiburi au hata kupuuza sharia za Mungu kama zinavyofunuliwa kwenye Biblia. Kumbuka, sio kiwango cha ukengeufu inachosababisha dhambi, bali ukengeufu wenyewe ambao unaleta uharibifu wa rohoni. Ni kwa nini? Kwa sababu hata maelewano madogo kwa dhambi yanathibitisha kuwa ubinafsi, na sio upendo kwa Yesu, ndio nguvu inayotawala maishani. Kwenye hali kama hizi, kamwe utu wa kale haujafa. Alibatizwa, lakini akazikwa akiwa hai.

Hii ndiyo hatari ya kufundisha kuwa wokovu unafanyikia msalabani. Kwa matokeo ya fundisho hilo la uongo, ni mamilioni ya watu ngapi ambao wataamka baada ya miaka elfu moja, wakiwa upande usiofaa wa ufufuo? Wakiwa wameshtuka na kushangaa, watasema: "Bwana, Bwana... hatukufanya… kwa jina lako miujiza mingi?" Mathayo 7:22. Na Yesu atawatangazia hivi: "Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu." Mathayo 7:23.

Kuwa kwenye hali hii kwa hakika ni hali ya Walaodokia; watu wanaodhani kuwa wao ni matajiri na wana mali nyingi na hawana haja ya kitu kingine chochote. Kielelezo hiki kinaonesha kuwa yale waliyoyapitia yalikuwa ni kwa lengo la kuonekana tu. Ijapokuwa, endapo kitabu cha Waebrania 9:27 kinaeleweka kama ipasavyo, kuna tumaini kubwa sana kwa Mkristo.

> “Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu;” Waebrania 9:27

Hukumu yako haifanyiki baada ya kumpokea Kristo na kuziungama dhambi zako. Hukumu yako inafanyika baada ya wewe kufa. Haijalishi unakiri nini wakati ukiwa hai kwa sababu maisha yako bado yapo chini ya uangalizi, dhambi zako bado zipo kwenye kumbukumbu, na unaweza kugeukia upande mmoja au mwingine. Kwa hivyo, hukumu hufanyika baada ya wewe kufariki na sio ukiwa hai. Kujua jambo hili ni kitu chema kwa sababu inamfanya mtu awe muangalifu zaidi na kuelewa zaidi msimamo wake wa kweli mbele za Mungu.

Kwenye kielelezo kilichotolewa hapo awali, kuna uwezekano mkubwa sana kwamba kanisa lingedai kuwa kwa vile mtu huyo alikuwa anafanya vizuri basi angeokolewa; na hivyo mtu mwenye dhambi pia angeamini kuwa amekubaliwa kuingia mbinguni na hana haja ya kitu kingine chochote. Hali halisi ni kuwa, mtu huyo anahitaji kujua kuwa yeye ni mwenye dhambi na kama ataendelea kuwa kwenye dhambi basi ana hakika kuwa amepotea.

Dhabihu isiyo na kipimo ya Kristo haiwezi kumsaidia mtu yeyote endapo ataendelea kuwa kwenye dhambi baada ya kupokea maarifa ya ile kweli ipasayo. Kwa hakika, kulingana na kitabu cha Waebrania 10:26-27, msalaba utamhukumu mtu huyo, sio kumuokoa.

> “Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi;
>
> bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.” Waebrania 10:26-27

Je, ni nini kinatokea kwa mtu ambaye, baada ya kupokea maarifa ya injili, anaendelea kutenda dhambi kwa makusudi? "Haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Hata hivyo, kinachosalia ni "kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao." Mtu anayetenda dhambi kwa makusudi baada ya kuupokea msalaba anakabiliwa na hukumu ya kutisha na hasira kali. Ni wazi kuwa hakuokolewa pale msalabani!

Enyi marafiki, ni nini kingine ambacho Mungu anaweza kutufanyia pale tunapokiri kuikubali injili na bado tukaendelea kufanya dhambi? Paulo anajibu swali hili kwenye kitabu cha Waebrania 10:29.

> "Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema." Waebrania 10:29

Kutenda dhambi kimakusudi baada ya kupokea ujuzi wa ile kweli ipasayo ni jambo la kutisha sana kama Paulo anavyoelezea kwenye mstari unaofuatia.

> "Maana twamjua yeye aliyesema, Kupatiliza kisasi ni juu yangu, mimi nitalipa. Na tena, Bwana atawahukumu watu wake." Waebrania 10:30

Injili hii ya uongo ya kwamba 'ukishaokolewa, basi umeokolewa daima' inahusisha mtu kufanya dhambi kabla ya msalaba na bado anatenda dhambi baada yake. Ila kulingana na kitabu cha Waebrania 9:27, nafsi huhukumiwa baada ya kufa, na hivyo hukumu ya Kimungu inasema wazi kwamba amepotea kwa sababu mpaka kifo chake, bado alikuwa akitenda dhambi!

Hebu sasa tuiangalie injili ya kweli. Fikiria kabla ya mtu kubadilishwa (kabla ya kuupokea msalaba). Yeye anakuwa ni mwenye dhambi na maisha yake yanatawaliwa na kuipenda zaidi nafsi yake. Wakati fulani hapo baadaye, anasikia injili. Anajua hali yake na kwa unyenyekevu na

roho iliyo tayari kutubu anakwenda kutubu, kuungama dhambi zake, na kusamehewa. Kwenye hatua hii ya mfano, utu wa kale unakuwa umekufa. Mtu ambaye alikuwa ndani yake kabla ya wakati huu hataishi tena. Maisha makamilifu ya Kristo sasa yanaishi ndani yake. Baada ya kuupokea msalaba, anatembea kwenye uzima mpya, kama tunavyosoma kwenye kitabu cha Warumi 6:4.

> "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake; kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima." Warumi 6:4

Baada ya kifo cha mtu huyu, maisha yake yanapitiwa upya kabla ya hukumu, na anahesabiwa kuokolewa. Hii ndiyo injili ya kweli! Ni rahisi sana.

Kwenye kitabu cha Wakolosai 3:3 tunasoma hivi: "Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu." Hii ndiyo haki ya kweli kwa imani. Hivi ndivyo namna ambavyo mwizi aliokolewa pale msalabani. Mtu huyo alikufa msalabani kabla ya mapigo ya moyo wake kuacha kudunda. Alipokea msamaha na akawa mtu mpya; ambaye maisha yake yalifichwa pamoja na Kristo kwa Mungu, hata kama ilikuwa ni kwa muda mfupi tu.

Sasa kifikirie kitabu cha Warumi 8:11.

> "Lakini, ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu." Warumi 8:11

Paulo anasema kuwa utukufu wa Baba aliyemfufua Yesu kutoka kwenye wafu pia utaihuisha miili yetu kwa Roho Wake. Hii ndiyo sababu baada ya kubatizwa, maisha ya mwenye dhambi sio tu kwamba yanayaboresha mambo ya kale, bali ni kuwa yanakiunda kiumbe kipya kabisa.

Je, umeona namna kitabu cha Warumi 8:11 kinavyoulinganisha ufufuo wa Kristo na nguvu Aliyoipokea, na nguvu ambayo mtu anayeamini anaipokea kwenye nafsi yake pale anapokufa na kufufuliwa kwenye uzima mpya? Paulo analilinganisha jambo hili sawasawa kwenye kitabu cha 1 Wakorintho 6:14:

> "Naye Mungu alimfufua Bwana, na tena atatufufua sisi kwa uweza wake." 1 Wakorintho 6:14

Kuna vifungu vingi sana vinavyolifafanua jambo hili kwa kiina. Kwa kweli, Mungu anataka tuuelewe ukweli huu mzuri, kuwa Atatuinua kwa nguvu zile zile Alizomfufua Mwanawe, Yesu Kristo.

Kristo alipomfufua Lazaro kutoka kwenye wafu, haikuwa tu ni kielelezo cha ufufuo wa watakatifu, bali ulikuwa ni ufufuo wa mtu anayeamini pale anapozaliwa mara ya pili. Kwenye huu mfano pia, roho hupokea uzima wa kiroho, na maisha ya zamani yanabakia pale kaburini. Sister White anaongezea mkazo zaidi juu ya hili kwenye *The Desire of Ages*.

> “Mfungueni, muacheni aende zake… Lazaro yupo huru, na amesimama mbele ya umati, si kama mtu aliyedhoofika kwa ugonjwa, na viungo vilivyolegea, bali kama mtu mdogo kabisa, na kwenye nguvu za maisha na utu uzima. Macho yake yanang’aa kwa akili na upendo kwa Mwokozi wake.” {DA 536}

Kufufuka kwa Lazaro kunatoa ushuhuda wa uwezo wa ufufuo wa kumuumba upya mtu mwenye ugonjwa uliosababishwa na dhambi na kumrejeshea nguvu, ari, heshima na upendo kwa Yesu moyoni. Kila kitu ambacho Yesu alimfanyia Lazaro kwa kumuita kutoka kaburini kinatokea kwa mtu anayeamini hasa pale anapoyapitia mabadiliko. Anarejeshwa kwa nguvu mpya, akili, na ari nzuri zaidi, na zaidi ya yote, anafanywa upya kwenye uchaji na maarifa na upendo kwa Mwokozi wake. Kama vile Lazaro alivyotoka kaburini akiwa hana maradhi, na kutembea kwa nguvu za utu uzima, vivyo hivyo ndivyo mwenye dhambi aliyetubu hutoka kwenye kaburi lililojaa maji (ubatizo) akitembea kwenye uzima mpya.

Kwa kupendeza sana, jina la Lazaro kwa Kigiriki lina maana ya Eleazari. Neno El linamaanisha Mungu na neno Azar linamaanisha kusaidiwa. Kwa hiyo, Lazaro anatafsiriwa kuwa ni: 'mtu anayesaidiwa na Mungu.' Pia, Mungu anataka kutusaidia, kutufufua tukiwa huru kutoka kwenye wafu na unajisi wa dhambi.

Je, ni nini kilichomfufua Lazaro kutoka kwenye wafu? Lilikuwa ni neno la Kristo lililonenwa kama inavyooneshwa kwenye kitabu cha Yohana 6:63. Hapa, Yesu anasema:

> "Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima." Yohana 6:63

Maneno ambayo Yesu aliyasema yaliupa uhai mpya mwili wa Lazaro. Nini maana ya maisha mapya? Tunapata jibu kwenye kitabu cha Warumi 8:2.

> "Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti." Warumi 8:2

Lazaro alipokea maisha ya Kristo Yesu. Pia, Paulo alisema: "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu;" Wagalatia 2:20. Uhai wa Kristo huishi ndani ya mtu aliyekuwa akitenda dhambi na kuwekwa huru, na hivyo Kristo anaweka "uhai mpya". Hata hivyo, hauwezi kupata ufufuo huu wakati utu wa kale ukiwa bado unaishi. Hapo ndipo watu wengi wanadang'anywa. Kushiriki maisha ya Kristo haihusiani na suala la muda gani umekaa kanisani, ni safari ngapi za umisheni ambazo umezifanya, au ni mahubiri mangapi ambayo umeyahubiri. Maadamu utu wa kale ungali hai, mtu hatakiona kile tunachojifunza hapa kuhusu ufufuo. Ni lazima utu wa kale ufe kabla ya kupewa maisha mapya. Huu ni ukweli wa injili na iwe ni kama tunakubaliana nao au laa, tunaamini au hatuamini—utu wa kale hauna budi kufa endapo tutafufuliwa kwenye ufufuo wa kwanza.

Fikiria kitabu cha 1 Wakorintho 15:36 ambapo, akizungumzia ufufuo wa watakatifu, Paulo anasema hivi: "Ewe mpumbavu! Uipandayo hai-

huiki, isipokufa." Utu wa kale usipokufa hauwezi kuwa ni kiumbe kipya. Angalia kile ambacho Yesu anasema kwenye kitabu cha Yohana 12:24-25:

> "Amin, amin, nawaambia, Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali hiyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi.
>
> Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele." Yohana 12:24-25

Ili mmea ukue na kuzaa matunda, ni lazima mabadiliko yafanyike kwenye mbegu. Kwa kweli, ni lazima mbegu ipoteze uhai wake. Hauwezi kuwa na mmea wakati mbegu inabakia kwenye hali yake ya kutokuota. Vivyo hivyo, maadamu mtu wa kale angali hai, hatoweza kuzaliwa tena kwenye uumbaji mpya, na hatatokea kwenye ufufuo wa kwanza. Badala yake, unabakia kuwa ni utu ule ule wa kale na atakuja kufa kifo cha mara ya pili. Yesu alisema hivi: "Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele." Tunapaswa kuyachukia maisha ya dhambi ambayo tumeyaishi. Ni lazima tuiue nafsi ya mwanzo ili tuwe na maisha mapya sasa na hata kwenye ulimwengu ujao. Na kifo cha utu wa kale, kwa nafsi yake, daima ni kujisalimisha; sio uamuzi wa mara moja tu. Inatokea mara kwa mara.

Sasa ona kile ambacho Paulo anasema kwenye kitabu cha 2 Wakorintho.

> "Siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. Kwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti." 2 Wakorintho 4:10-11

Inatupasa kuisalimisha asili ya kimwili ili uzima wa Kristo udhihirishwe kwenye miili yetu ipatwayo na mauti. Kwenye huu mchakato wote,

mapenzi yako wewe mwenyewe ni nguvu inayoongoza. Kabla na baada ya uumbaji mpya, kamwe ukweli huu haubadiliki. Sio asili yako inayotawala, kwa sababu kama tulivyojifunza kwenye masomo yaliyopita, asili yako sio dhambi. Mwili wenyewe hauwezi kutenda kinyume na mapenzi ya Mungu. Ni mapenzi yako ndiyo yanayokufanya ujisalimishe.

Roho Mtakatifu anapousukuma moyo wako, unaweza kuchagua kutorejea kwenye maisha yako ya zamani. Kisha, Mungu Atakubariki kwa nguvu za ufufuo. Kwa hakika, nguvu hiyo hiyo iliyomfufua Yesu kutoka kwenye wafu itakufufua wewe ili uishi kwa ushindi na kuleta heshima Kwake. Walakini, ni mapenzi yako ambayo huamua juu ya jambo hili. Ni lazima wazo hilo ovu na matendo hayo maovu yapotezwe.

Kwenye maandiko matatu yanayofuata unaona ni mara ngapi Paulo anavyolitumia neno 'mavuno', kuhusiana na mapenzi na maamuzi ambayo mtu huyafanya yeye mwenyewe.

> “Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki.”
> Warumi 6:13

Hii ndio sehemu tunayowajibika kuhusika nayo. Mungu hutoa ushindi na nguvu, lakini ni juu yetu kuyatoa mapenzi yetu Kwake Yeye. Mungu alimuumba mwanadamu kwa hiari yake, na hataiondoa hali hiyo. Ataheshimu hiari yetu haijalishi iwe inatupeleka jehanamu, au kama Apendavyo Yeye, inatupeleka mbinguni. Enyi marafiki, kila mtu anayeenda mbinguni atakuwa huko kwa sababu alitaka kwenda huko. Tunao uwezo wa kuchagua uzima wa milele—tazama ni nguvu gani ya ajabu ambayo Mungu ameiweka kwenye mikono yetu sisi wenyewe!

Andiko letu la pili ni kutoka kitabu cha Warumi 6:16:

> “Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii; kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au

> kwamba ni utumishi wa utii uletao haki." Warumi 6:16

Andiko la tatu ni kutoka kitabu cha Warumi 6:19:

> "Nasema kwa jinsi ya kibinadamu kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu. Kwa kuwa kama mlivyovitoa viungo vyenu vitumiwe na uchafu na uasi mpate kuasi, vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki mpate kutakaswa." Warumi 6:19

Kila dakika ya kila siku, tunapaswa kuyaachilia mapenzi yetu na kuamua kuwa watumishi wa haki. Kila siku tunapaswa kuusalimisha utu wa kale na matendo yake, daima tukifa pamoja na Bwana Yesu ili uzima Wake udhihirike ndani yetu.

## SURA YA 5

Kuna swali ambalo ni la muhimu na linahitaji majibu. Yesu alipokufa msalabani, ni nini ingine iliuwawa?

Dhambi zetu. Dhambi za kila mtu ambaye amewahi kuishi au atakayeishi ziliuawa pale msalabani. Hiki ndicho anachokisema Paulo kwenye kitabu cha Warumi 6:10—"Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu." Maisha ya Yesu ya kujitoa dhabihu, yalifikia kilele pale msalabani, na yaliilipia kila dhambi ambayo imewahi kutendwa. Lakini Kristo, Asiye na dhambi, hakulipa dhambi zetu pekee, Aliziangamiza. Alitoka kaburini akaishi kwa ajili ya Mungu Baba Yake, kama Alivyofanya kabla ya kifo Chake.

Kwenye kitabu cha Warumi 8:3 tunaona kuwa Yesu "aliihukumu dhambi katika mwili". Hii inamaanisha kuwa Yesu alishinda dhambi, na hivyo dhambi iliharibiwa. Kwa sababu hii, hakuna mtu anayepotea. Na sio tu kwa sababu dhambi zetu zimelipiwa, bali ni kwa sababu hatuhitaji tena kuwa watumwa wa dhambi hizo. Ingawa bado zipo kwenye kumbukumbu kwa sababu mahali patakatifu bado hapajatakaswa, nguvu za dhambi zako zimeharibiwa, na kwa hivyo hakuna tena haja ya dhambi kutufanya watumwa. Anacho takiwa kufanya ni kufanya mapenzi ya Mwokozi wako.

Yesu alitokaje kaburini? Je, kulikuwa na madhara yoyote ya dhambi juu Yake? Hapana. Kama ambavyo tumeona kwenye sura iliyotangulia, Yesu alikuja ili kutukuzwa; alikuja bila alama ya dhambi hata kidogo. Hakika, Yesu alizilipia na kuzilaani dhambi za wanadamu wote, na akaziacha kule kule kaburini. Nguvu ya ufufuo ilidhihirika na mwanadamu aliyetukuzwa alitoka nje ya lango la kaburi.

Bila shaka, wakati Lazaro alipotoka kaburini bado alikuwa ni mwenye kustahili kufa, asili yake ya ubinadamu iliyoanguka ilikuwa haijabadilika, lakini alifufuka "kama mtu mdogo kabisa, na kwenye nguvu za maisha na utu uzima… [aking'aa] kwa akili na upendo kwa Mwokozi wake." {DA 536} Lazaro alitembea kwenye upya wa uzima akiwa ni kama kiumbe kipya ingawa bado alikuwa ameanguka; ufufuo wake

ulifananishwa na tukio la kuzaliwa kwa mara ya pili.

Kumbuka maneno ambayo Yohana Mbatizaji aliyasema kwenye kitabu cha Yohana 1:29: “Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwenguni.” Yesu aliichukua dhambi ya ulimwengu wote pale msalabani.

Fikiria kwa muda kuhusu utu wa kale na dhambi zake zinazosumbua, bila ya kujali zikoaje. Je, unaweza kumtenga mtu na dhambi zake? Hapana, haiwezekani. Dhambi huzaa tabia mbaya ambayo humuelezea mtu kuwa yeye ni wa aina gani. Kwa kweli, kwa kawaida mtu huwa anafahamika kwa kupitia dhambi zake. Mtu anayesema uongo anajulikana kuwa yeye ni muongo. Mtu anayekashifu anajulikana kuwa yeye ni mtu anayekashifu. Anayezini ni mzinzi, na anayeua ni muuaji.

Dhambi hutengeneza tabia ya dhambi; inakuwa ndiyo wewe hasa. Ndio maana hauwezi kuutenga utu wa kale na dhambi zake. Inatakiwa kwanza uiue nafsi ya kale, na unapofanya hivyo, unaziua dhambi ambazo ni sehemu yake. Muongo hawezi kusema uongo baada ya kufa. Hawezi kuendelea kuishi baada ya kuupokea msalaba. Lazima kuwe na mtu mpya ndani yake, ama sivyo bado utakuwa na matatizo kama yale uliyoyapata hapo awali. Au kwa njia nyingine, unakuwa kama Walaodokia, waliodanganywa kwa kufikiri kuwa kwa sababu unafanya dhambi kidogo, basi unaenda mbinguni.

Watu wengi sana wanaangukia kwenye mtego huu, wakiamini kuwa kwa sababu wana mienendo mizuri na wanafanya mambo mazuri basi wao wataokolewa. Wokovu wao unategemea matendo. Hata hivyo hawana tofauti na jinsi walivyokuwa hapo awali; bado wanakengeuka kutoka kwenye matakwa ya Mungu, ukiangazia ukweli kwamba ubinafsi bado inawatawala.

Tazama jinsi Biblia inavyouunganisha utu wa kale na dhambi zake.

> “Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya.” Waefeso 4:22

Utu wa kale umeharibika na umejaa tamaa za udanganyifu. Dhambi na mtenda dhambi wanakwenda pamoja. Ni lazima utu wa kale uvuliwe. Ukweli huu umeelezwa wazi kwenye kitabu cha Wakolosai 3:8,9:

> "Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake;" Wakolosai 3:8,9

Utu wa kale na matendo yake huenda pamoja, na hivyo, hufa pamoja.

Ni muhimu kuelewa uhusiano kati ya muumini na Kristo, hasa kwenye suala la kusulubishwa na ufufuo Wake. Wakati mwenye dhambi aliyetubu anapoamua kwenda kubatizwa, anapaswa kuamini, si tu kuwa dhambi zake zililipiwa pale msalabani, bali kuwa dhambi zake zilisulubiwa pale msalabani. Kitabu cha Warumi 6:6 kinasema hivi:

> "Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena." Warumi 6:6

Ubatizo ni ushuhuda wa hadharani ya kuwa utu wa kale na matendo yake yameharibiwa. Hii inafikiwa kwa imani kwa Kristo, ambaye aliiharibu dhambi kwa kusulubiwa na ufufuo. Kwa njia ya mfano, kubatizwa pamoja na Kristo maana yake ni kusulubishwa pamoja Naye pale Kalvari.

Dhambi za wanadamu wote zilipelekwa kwenye kaburi la Yusufu, na hivyo ndivyo utu wa kale na matendo yake yanavyozikwa kwenye maji ya ubatizo na kuna ufufuo mpya wa uzima. Ndiyo maana Kristo alisema hivi: "Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu." Yohana 3:5. Isipokuwa mtu amebatizwa na kwa mujibu wake, anazilipia dhambi zake pamoja na Kristo pale mtini, atalipia dhambi zake kwenye kifo cha pili. Hakuna anayeweza kuepuka sheria ya Warumi 6:23, kwamba "mshahara wa dhambi ni mauti". Kama vile nabii Ezekieli alivyosema, "roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa." Ezekieli 18:20.

Hata hivyo, kwenye kitabu cha Warumi 6:6, Paulo anatufundisha kuwa, kama mtu atabadilika kweli, basi "utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena". Hii aya inathibitisha wazi kuwa baada ya kubadilishwa, muumini hahitaji tena kuwa mtumwa wa dhambi. Tena, hivyo ndivyo Paulo anavyosema kwenye kitabu cha Wagalatia 2:20: "Nimesulubiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu."

Paulo aliishi nyakati za Yesu, na sisi tunaishi miaka elfu mbili hivi baada ya Yesu, lakini hakuna tofauti. Kwenye kitabu chake cha Glad Tidings, Wagoner anaangazia sana jambo hili. Hatupaswi kulifikiria tukio la Kalvari kama ni tukio la mbali ambalo lilifanyika miaka elfu mbili iliyopita. Kalvari ni jambo la sasa hivi na pia ni la kulizoea wakati huu kwenye maisha yako. Kufa kwa mwili wa Bwana Yesu ni jambo ambalo hutokea kila siku kwa kila dakika. Unapaswa kuelewa kuwa Alikufa kwa ajili ya dhambi zako; Aliziharibu dhambi zako, na Anafanya hivyo kwa ajili yako hata sasa hivi.

Sitajali kuwa umefanya kitu gani, kama umekuwa gerezani au umefanya mauaji, Yesu alikufa na dhambi zako ziliharibiwa. Dhambi haipaswi kuwa na nguvu zaidi juu yako. Kristo aliiangamiza dhambi na wewe hauna tena haja ya kuitumikia. Hii ndiyo habari njema ya injili! Kwa imani, anayebatizwa anaamini kuwa utu wa kale na matendo yake yamesulubishwa pamoja na Kristo. Mwili huo wa dhambi unakufa, na sasa kuna mtu mpya ambaye pamoja na Paulo wanaweza wakasema hivi: "Nimesulibiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu." Wagalatia 2:20.

Marafiki, je, mtu aliyekufa anaweza kutenda dhambi? Andiko la kitabu cha Warumi 6:7 linasema hivi: "kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi." Tunahitaji kuufikiria utu wetu wa kale kuwa umekufa; ni lazima sisi tujiambie hivi kila mara. Mwandishi wa *The Power of Positive Thinking* hakuwa Norman Vincent Peale—alikuwa Mungu, alikuwa Yesu, na alikuwa mtume Paulo. Biblia imejaa mawazo nyingi. Mungu huona mema ndani ya mwanadamu na huyatoa ndani yake. Yesu alimuona mtoza ushuru, mwizi lakini aliona pia mema ndani ya mtu huyo, Akavuta dhambi kwake akamshindia mtu huyo milele.

Simoni alikuwa ni Mfarisayo mwenye kiburi ambaye siku zote alikuwa akiwahukumu wengine, lakini Yesu aliona kitu ambacho ange vuta kutoka kwake; Alimuona kuwa ni mwanafunzi anayejishusha, aliyejitoa sadaka. Yesu alikuwa na kipaji kizuri zaidi cha kuona mema ndani ya mtu na kudhihirisha wazi. Kwa hiyo, inatupasa kuwatazamaje wengine ambao wameumbwa kwa mfano Wake, wakati Mungu anawatazama kwa uwezo mkuu sana?

Tunahitaji kuibua taswira ya utu wa kale ukiwa umekufa na kwa hiyo tukiri kuwa hauwezi kutenda tena dhambi. Kama vile Paulo anavyoandika kwenye kitabu cha Waefeso 4:24, "mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika uadilifu na utakatifu wa kweli."

Tazama jinsi Paulo anaelezea kwenye Waefeso 2:10:

> "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo." Waefeso 2:10

Mungu alikuwekea maisha ya ushindi tangu pale ulipozaliwa. Anaona mema ndani yako, anaona uwezekano wa wewe kuumbwa kwa Kristo Yesu kwenye haki na utakatifu. "Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo." Wagalatia 3:27

Hebu sasa turejee kwenye kitabu cha Warumi 6:10 ambapo tunasoma hivi:

> "Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu." Warumi 6:10

Sababu ya Paulo kutumia neno "mara moja tu" hapa ni muhimu sana. Dhabihu ya Yesu ilitosha kuharibu dhambi milele, mara moja na moja kwa moja. Alikuja kutoka kaburini bila aina yoyote ya dhambi; Aliilaani dhambi kwenye mwili.

Leo, na kwenye umilele wote, Anaishi kwa ajili ya Mungu na Anaishi kwa ajili yetu. Hiki ndicho anachokipitia Mkristo aliyebadilishwa kama

tunavyoona kwenye mstari unaofuatia. Paulo amemaliza tu kutuambia jinsi ambavyo Yesu alikufa kwa dhambi mara moja, na jinsi anavyoishi kwa ajili ya Mungu, kisha neno linalofuata analosema ni "vivyo hivyo."

> "Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi." Warumi 6:11

Neno "jihesabuni" kwenye aya hii ina maana ya kuhitimisha; kujiona kuwa wewe ndiwe mwenyewe. Paulo alituambia kuwa dhambi zetu ziliharibiwa pale msalabani, kuwa zililipiwa, zilihukumiwa na kuharibiwa. Vivyo hivyo, anasema, jiamini wewe mwenyewe kuwa umekufa kwa dhambi na kwamba sasa u mtu mpya anayeishi kwa Mungu. Kile ambacho Kristo alikipitia, Alikipitia kwa ajili yetu. Tunaamini hili kwa imani na tunaweza kuyapata maisha yale yale.

Hii ni muhimu kwa sababu kuna makundi mawili tu. Una utu wa kale ambao utapotea na una mtu mpya ambaye anaenda kuokolewa. Hakuna mtu wa kati. Haina uhusiano wowote na dini, kanuni za imani au kitu kingine chochote kile. Makundi mawili tu; kuokolewa na kupotea. Utu wa kale ukibakia, basi unakuwa umepotea. Ukiyapitia maisha ya "mtu mpya" mpaka kifo, unakuwa umeokolewa. Utu wa kale unaishi kwa ajili yake wenyewe, mtu mpya anaishi kwa ajili ya watu wengine. Utu wa kale umeharibika, kwa kufuata tamaa yenye udanganyifu. Mtu mpya anaumbwa kwenye haki na utakatifu wa kweli. Tazama ambavyo Paulo anasema "utakatifu wa kweli".

Siwezi kusisitiza vya kutosha jinsi ambavyo kitabu cha Warumi 6:11 kinaweza kuleta mabadiliko. Paulo anatuambia tujihesabu kuwa wafu kwa dhambi lakini walio hai kwa Yesu Kristo. Sasa angalia anachokisema kwa Warumi 10:10:

> "Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki; na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu." Warumi 10:10

Paulo hasemi uwe na imani ya kupata haki kwa matendo yako ya hisani, au kwa kuwalisha watu maskini. Bali, ni pale unapoamini kwa moyo kuwa utapata haki, na kwa kinywa chako ukakiri kupata wok-

ovu. Unaweza kulipitia jambo hili sasa hivi kwa sababu halina uhusiano na kile unachokifanya. Ingawa ni matendo yanayothibitisha imani yako, sidhani kama kuna mstari mwingine kwenye Biblia nzima unaoharibu Uyahudi au 'haki kwenye matendo' kama huu hapa. Wokovu unategemea kile unachokiamini na kile unachokiri. Inashangaza sana hii! Unachokiamini moyoni mwako na unachokikiri kwa kinywa chako kinakuletea haki na wokovu, kisha matendo hufuatia. Ndiyo maana Paulo anatuambia "jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi". Hauna budi kuliamini jambo kwanza, na kisha litafanyika.

Mama yangu alipokuwana muda wa wiki chache za kuishi duniani, niliketi pamoja naye nikiwa pamoja na binti yangu nyumbani kwake, kabla tu hatujampeleka hospitalini kwa mara ya mwisho. Hakukuwa na kitu chochote ambacho kilibakia kwake. Mama aliniuliza kwa Kiitaliano juu ya kile alichopaswa kukifanya ili kwenda sawa sawa na Mungu. Hakukuwa na muda wa kuanza kupitia masomo ya muda mrefu sana. Alikuwa ni mdhaifu sana na hakuwa na hata uwezo wa kufikiria kwa kiasi kikubwa sana. Lakini swali hilo lilitoka kwake, na sio mimi. Hata sikuwa nikijaribu kumhimiza afanye hivyo. Nilijua kuwa Mungu alikuwa akimuongoza hivyo nikamuuliza kama anaamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zake. Alijibu akasema Ndiyo. Kisha nikamsomea mstari mmoja: Warumi 10:10. Mstari tuliotoka kuutazama hivi sasa. Siwezi kufikiria mstari wenye nguvu zaidi au mzuri zaidi kwenye Biblia nzima wa kumsomea mtu yeyote kwenye hii hali—anayekabiliwa na kifo. Nikamuambia: "Mama, kwa moyo wako unaweza ukaamini na ukapata haki, na kwa kinywa chako unaweza ukakiri na ukapata wokovu." Ni Mungu tu ndiye ajuaye kile ambacho kilikuwa moyoni mwa mama yangu, lakini tukio hilo lilinijaza tumaini la ajabu sana.

Enyi marafiki, daima Imani huja kabla ya matendo. Inabidi kwanza uamini kwamba ule utu wa kale umekufa kwa dhambi maana ndivyo ambavyo mstari unasema. Kujihesabia, ni kuhitimisha, kufikiria au sababu. Biblia inakuambia uhitimishe kuwa umeifia dhambi, kuwa utu wako wa kale ulikufa kabisa pale msalabani, mara moja na moja kwa moja. Angalia kitabu cha Warumi 6:11 tena na uangalie mkazo unaotumika. Paulo hasemi tu jihesabuni kuwa wafu, bali "wafu kweli" kwa ajili ya dhambi. Paulo anasisitiza jambo hili sana. Kazi yako ni kuamini.

Kumbuka, kuna makundi mawili tu. Aidha wewe una utu wa kale, ambayo ina maana kuwa umepotea, au wewe ni mtu mpya, aliyeumbwa kwa Kristo Yesu. Kama unajihesabia kuwa umekufa kwa dhambi, basi nini kinachopaswa kufuatia hapo? Angalia mstari unasema nini —"walio hai kwa Mungu, katika Kristo Yesu."

Mwizi alikuwa akifariki akiwa msalabani baada ya kuwa ni mhalifu; alikuwa amevunja sheria ya maadili na ile ya kiraia na alisimama kwenye ukingo wa laana ya milele. Anaponing'inia kwenye msalaba huo akikaribia kufa, anajua kuwa ana hatia na kuwa hakuna mwizi anayekwenda mbinguni. Anachoweza kufanya ni kuamini moyoni mwake kwa wema kama vile ambavyo kitabu cha Warumi 10:10 kinavyosema. Hawezi kufanya jambo lingine lolote. Uthibitisho wa Biblia unasema: “Na sasa, namna dhambi yote ilivyochafuliwa, historia ya maisha yake ipo karibu kufungwa”. {DA 750}

Anakaribia kukutana na hatma yake na maisha yake yamechafuliwa na dhambi. Anaweza kufanya nini? Hawezi kushuka kutoka msalabani na kuanza kurekebisha maisha yake. Hawezi kurekebisha mambo yake mabaya.

Enyi marafiki, mtu huamini kwa moyo na kupata haki. Hapo anachoweza kufanya huyo mwizi ni kuamini. Anakufa na hawezi kufanya jambo lingine lolote. Inampasa ajihesabie kuwa mfu kwenye dhambi; hana budi kuamini kuwa yeye ni mtu mpya kwenye haki kwa sababu hakuna mwizi atakayeingia mbinguni. Anakiri imani yake na kusema hivi: “Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako” Luka 23:42. Na siku hiyo mtu huyo aliokolewa. Imani yake ilimuokoa, kwa maana Yesu anasema hivi kwenye mstari unaofuatia: “Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi.” Luka 23:43. Wakati huo huo mwizi anasimama mbele za Mungu akiwa ni mtu mpya, aliyekubaliwa kwa Mpendwa. Mkosaji aliyekuwa mbaya zaidi ambaye anaamini kweli, wakati huo anapokea msamaha kutoka kwa Yesu. Sehemu zote kwenye Biblia, kuna matukio mengi sana ambapo Yesu anageuza hali mbaya kuwa wokovu wa milele—tazama ni jinsi gani upendo wa Mungu ulivyokuwa ni wa ajabu hivi.

Angalia Uthibitisho wa Biblia unasema nini kuhusu mwizi msalabani kwenye The Desire of Ages: “Kwa mwizi aliyetubu alipatwa na amani iliyo kamilifu ya kukubaliwa na Mungu.” {DA 751}

Enyi marafiki, hili ndilo jambo la muhimu zaidi la kulihangaikia kwenye maisha haya. Sio utajiri, ardhi, umaarufu au kitu kingine chochote. Jitahidi kupata amani hii ambayo ni kamilifu ambapo hakuna tena kama hiyo. Mwizi alikumbana nayo. Ni lazima maumivu yake yalififia alipopata kibali kwa Mungu. Hii ni injili ya ajabu iliyoje! Hakuna mfano mkubwa zaidi kwenye haki kwa imani kwenye Biblia kuliko ile ya mwizi kuwa msalabani.

Unapoamini kweli kwenye kitabu cha Warumi 6:11—kuwa kweli u mfu kwa dhambi—lengo lako litakuwa ni kwenda mbinguni. Hili ndilo linalotufanya tusiurudie utu wa kale. Angalia kwenye mistari mitatu inayofuata juu ya namna ambavyo mtu wa kale anakufa na mtu mpya kufufuliwa pamoja na Kristo. Inaelekea Paulo alifundisha ukweli huu zaidi ya kitu kingine chochote alipoifafanua injili. Ndio sababu alikuwa na nguvu sana mbele ya Mataifa. Vifungu hivi vyote vinapatikana kwenye barua zake kwa makanisa ya Mataifa.

> "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu." Wakolosai 3:1

Hapo ndipo nguvu ya urafiki ipo. Wakati utu wa kale ukiwa umekufa, ni lazima umakini wako ubakie kwenye mambo ya juu. Kwa mara nyingine tena kwenye mstari wa 2, Paulo anaandika:

> “Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.” Wakolosai 3:2

Tazamia mbinguni, na sio hapa duniani. Je, ni mara ngapi unaona umakini wa wanaojiita Wakristo ukielekezwa kwenye mambo ya kidunia, iwe ni juu ya pesa au mambo mengine mengi? Wakristo wa kweli wataweka fikra zao kwa Kristo. Sasa tazama hivyo pale unapofufuliwa pamoja na Kristo, Paulo anasema:

> “Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo

katika Mungu." Wakolosai 3:3

Kwa mara nyingine tena tunaona kuwa utu wa kale umekufa. Haupo kwenye harakati za kufa. Haujatoweka kwa muda mfupi tu. Utu wa kale haupo tena. Maisha yako sasa yamefichwa pamoja na Kristo ndani ya Mungu na unatazamia kufika mbinguni.

Je, unajua ni kwa nini Paulo anatumia dhana ya kufichwa na Kristo? Unapokificha kitu, kinakuwa ni salama na hakiwezi kuibiwa. Wakati maisha yako yakiwa yamefichwa pamoja na Kristo, hakuna awezaye kuyaondoa. Yesu anasema kwenye kitabu cha Yohana 10:29 kuwa "hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu." Hakuna mtu anayeweza kukutoa kwenye mkono wa Baba Yake. Yesu anasema kuwa Baba Yake ni mkuu kuliko Yeye na kuwa maisha yako yamefichwa pamoja Naye kwa Mungu.

Kwenye kitabu cha 1 Wakorintho 3:23, Paulo anasema hivi: "Ninyi ni wa Kristo; na Kristo ni wa Mungu." Tunapoyakabidhi maisha yetu kwa Mungu, na kuamini kweli kuwa tumekufa kwa ajili ya dhambi, tunaanza kuyapitia maisha mapya na Kristo akiishi ndani yetu. Kisha, maisha yetu "yamefichwa pamoja na Kristo kwa Mungu" na hakuna mtu anayeweza kututoa kutoka kwenye mkono wa Baba Yake.

**AMINA**

Kwa taarifa zaidi:

www.earthenvessels.org.au
info@earthenvessels.org.au

# Je, kusulubiwa pamoja na Kristo kunamaanisha nini?

Kwa Kupigwa Kwake huanza kwa kuchunguza siku ya upatanisho kwenye Agano la Kale na maana yake kwa watu wa Mungu mpaka leo hii.

Kitabu kinaendelea kufichua mafundisho ya uongo ya kuwa 'ukishaokolewa, basi umeokolewa daima' pamoja na kujibu swali la muhimu: "Je, Kristo alikufa kifo cha aina gani?"

Na hatimaye, kitabu hiki kiliandikwa ili kufunua ukweli wa kina wa Wagalatia 2:20:

*“Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.”*

EARTHEN VESSELS
2 CORINTHIANS 4:7